Jumatano Aprili 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580928
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US




SportPesa
TZS. 1,198,475,840
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




## CAG akuta mabilioni fedha za mirathi BoT

UKURASA 4



# Dk. Mpango aanika mafanikio matano ya Muungano

• **Samia** asamehe wafungwa 3,826, Mwinyi asema umeendelea kuimarika... *Endelea ukurasa 2, 17, 18*



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizindua kitabu cha historia ya Muungano wakati wa maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar jijini Dodoma jana. Wengine ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia) na (kushoto) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo. **PICHA: OMR**

## Operesheni yawanasa 'Panya road' waliovunja nyumba 23

UKURASA 4

## 16,000 waomba ajira afya, elimu kila siku

UKURASA 3

**MICHEZO** **'USHINDI YANGA SI DAWA MAUMIVU'** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6




Majeneza yenye miili tisa ya waumini wa kanisa katoliki mkoani Njombe, waliofariki kwa ajali ya gari iliyotokea kijiji cha Igima, wilayani Wanging'ombe, wakati wa ibada ya kuaga, iliyofanyika katika kanisa la Mt. Joseph, mjini Njombe jana. Habari **Uk. 4**. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

# Mpango ataja mafanikio matano ya Muungano

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameeleza mafanikio matano yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, hususani kwenye nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiusalama na kiutamaduni.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya Sherehe za miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zilizoadhimishwa jijini hapa, Dk. Mpango alisema katika miongo zaidi ya mitano ya Muungano, Tanzania imepata mafanikio makubwa yanayoonekana katika nyanja zote za maisha ya Watanzania.

Dk. Mpango alitaja mafanikio la kwanza ni katika siasa na jamii na kueleza kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umesaidia kujenga taifa lenye watu wanaozungumza lugha moja.

Alisema kabla ya Muungano, nchi hizo mbili zilikuwa zinatumia sheria mbili za uraia na uhamiaji, baada ya Muungano huo suala hilo likaanza kusimamiwa na sheria moja.

Dk. Mpango alisema: "Wananchi wamekuwa na uwezo wa kwenda au kuishi sehemu yoyote iliyopo katika Jamhuri ya Tanzania pasipo kikwazo. Kwa mfano ukienda Sumbawanga utawakuta Wapemba, ukienda Unguja utawakuta Wachaga, Wamasai, Wasukuma."

Alibainisha pia kumekuwapo na mwingiliano wa kiutamaduni na vyakula, mitindo ya mavazi, michezo, sanaa, ngoma na kuoleana kwa pande mbili za Muungano.

"Mambo hayo yamesababisha Watanzania kuwa wamoja zaidi, hata katika nafasi za kisiasa na utawala tumeshuhudia viongozi wakitoka upande wowote wa Muungano na kuongoza au kushika mhimiri ya dola wa Jamhuri ya Tanzania," alisema Dk. Mpango.

Alitaja fanikio la pili kuwa ni kuimarika kwa hali ya ulinzi na usalama nchini kwa kipindi chote cha miaka 58 ya Muungano.

Dk. Mpango alisema utulivu na amani umetawala kwa kipindi chote na kuwezesha Watanzania kuendelea na shughului zao za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

"Watanzania wa pande zote mbili tumeweza kulinda uhuru wetu pamoja na Mapinduzi yetu matukufu ya Zanzibar. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kutoka Zanzibar na Bara vinafanya kazi kwa weledi mkubwa," alisema Dk. Mpango.

Faniko la tatu Dk. Mpango alitaja ni katika sekta ya elimu na ajira.

Alisema katika miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kumewawezesha wanafunzi kupata elimu pasipo na ubaguzi.

Pia, wanafunzi wa Zanzibar wamekuwa wakienda Bara kupata elimu, kadhalika wanafunzi kutoka Bara wamekuwa wakaienda kupata elimu Zanzibar katika ngazi yoyote wanayoitaka.

"Pande zote mbili zimepiga hatua kubwa katika shule za msingi na sekondari, vyuo vikuu na vyuo vishiriki vimezidi kuongezeka tofauti na kabla ya Muungano," alisema Dk. Mpango.

Alisema katika kuwezesha wanafunzi wa elimu ya juu kupata mikopo, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imekuwa ikitoa mikopo kutoka Bara na Zanzibar bila ubaguzi.

Vile vile, alisema kupitia Sheria ya Utumishi wa Umma namba nane ya mwaka 2002 pamoja na kanuni zake za mwaka 2003, kumekuwa na utaratibu wa wazi wa ajira kwa watumishi wa umma na kuondoa dosari zilizokuwapo.

Alibainisha kwamba serikali imekuwa ikitoa nafasi za ajira kwa usawa kwa pande zote mbili.

Dk. Mpango alisema: "Wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakipata ajira Bara, kadhalika wa Bara wanapata ajira Zanzibar. Tumekuwa na wanazuoni maarufu kutoka Zanzibar wanaokuja kufundisha Bara, kadhalika wanazuoni kutoka Bara wanakwenda Zanzibar kufundisha kwenye vyuo vikuu."

Alitaja fanikio la nne ni katika medani za kimataifa kuwa Tanzania imekuwa na manufaa makubwa kuanzia medani za kikanda hadi Umoja wa Mataifa (UN).

Alisema heshima ya Tanzania UN ni kubwa kutokana na mchango wake katika mapambano ya ukombozi wa baadhi ya matifa Afrika, kushiriki katika vikosi vya kulinda amani vya UN, Jumuiya ya Mendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), pamoja na utatuzi wa migogoro ya kisiasa katika nchi mbalimbali.

Alitaja fanikio la tano kuwa ni maendeleo ya kiuchumi, kwa kuwa katika miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wawekezaji wakubwa kutoka pande mbili hizo wamefanya biashara bila kubadilisha fedha.

Alisema pia wananchi wake wanafanya biashara katika masoko makubwa kama Kariakoo na Darajani.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alisema awali Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa unakabiliwa na kero kubwa 25.

Alisema mwaka 2020 serikali za pande mbili zilifanikiwa kutatua kero saba na kubaki 18.

Jafo alisema uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ulipoingia madarakani umefanikiwa kutatua kero 11 na kuweka idadi ya kero 18 kati ya 25 zilizotatuliwa na kubakia kero saba.

## Rais asamehe wafungwa 3,826

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesamehe wafungwa 3,826 yakiwa ni maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Injinia Hamad Masauni, msamaha huo ulitolewa wakati wa maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano.

Hata hivyo, hautawahusisha wanaotumikia kifungo chini ya sheria ya bodi za parole sura ya 400 sheria ya huduma kwa jamii sura ya 291 na kanuni za kifungo cha nje ya 1968.

Aidha, ilifafanua kuwa msamaha huo pia hautawahusisha wafungwa wa madeni.

Kwa mujibu wa Waziri Masauni, msamaha huo pia umetolewa kwa kuzingatia masharti 18 ikiwamo, wafungwa waliohukumiwa adhabu ya kifo ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 30 na kuendelea na wanaotumikia kifungo cha maisha ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 20 na kuendelea.

"Wafungwa wote wapunguziwe robo ya vifungo vyao baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu linalotolewa chini ya kifungu cha 49 kifungu kidogo cha kwanza cha sheria ya magereza sura ya 58, pia wafungwa hao sharti wawe wametumikia robo ya vifungo vyao na wawe wameingia gerezani kabla ya Februari 26 mwaka huu," alisema Masauni.

Sharti la nne ni wafungwa wagonjwa wenye magonjwa ya kudumu ambao wametumikia robo ya vifungo vyao na wapo kwenye hatua ya mwisho, huku akielekeza kuwa wenye ugonjwa huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uwenyekiti wa mganga mkuu wa mkoa na wilaya.

Sharti la tano ni wafungwa wazee wenye umri wa miaka 70 au zaidi ambao wametumikia robo ya vifungo vyao, huku akisisitiza kuwa umri huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uwenyekiti wa mganga mkuu wa mkoa na wilaya.

La sita ni wafungwa wakike walioingia gerezani wakiwa na watoto wanaonyonya, wasionyonya na wajawazito ambao wametumikia robo ya vifungo vyao.

La saba ni wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili ambao wametumikia robo ya vifungo vyao, na alisisitiza kuwa ulemavu huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uwenyekiti wa mganga mkuu wa mkoa na wilaya, na la nane ni wale waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia mika 10 na kuendelea.

La tisa ni wafungwa wanaotumikia adhabu kwa makosa ya kujaribu kuua ambao wamekaa gerezani kuanzia mika 10 na kuendelea, na la 10 ni wale wanaotumikia adhabu kwa makosa ya kujaribu kujiua ambao wamekaa gerezani kuanzia mika 10 na kuendelea.

Sharti la 11 ni wafungwa wanaotumika adhabu kwa makosa ya kuua watoto wachanga ambao wamekaa gerezani kuanzia mika 15 na kuendelea, na sharti la 12 ni wanaotumikia adhabu kwa makosa ya uhujumu uchumi ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 20 na kuendelea.

Sharti la 13 ni wafungwa wanaotumikia adhabu kwa makosa ya matumizi mabaya ya madaraka yao ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka mitano na kuendelea, na la 14 ni wanaotumikia adhabu kwa makosa ya utakatishaji wa fedha ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 20 na kuendelea.

Sharti la 15 ni wafungwa wanaotumikia adhabu kwa makosa ya rushwa ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 10 na kuendelea, na la 16 ni wanaotumikia adhabu kwa makosa ya usafirishaji wa dawa za kulevya ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 20 na kuendelea.

Sharti la 17 ni wafungwa wanaotumikia adhabu kwa makosa ya utekaji au wizi wa watoto ambao wamekaa gerezani kuanzia mika 10 na kuendelea, na la 18 ni wanaotumikia adhabu kwa makosa ya wizi au ubadhilifu wa fedha na mali za umma ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 15 na kuendelea.

# Zaidi ya maombi 16,000 ajira afya, elimu hupokelewa kwa siku

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema hadi juzi maombi ya ajira yaliyopekelewa kikamilifu kwa kada ya afya na ualimu ni 83,514 kwa siku tano ikiwa ni wastani wa waombaji 16,703 kwa siku.

Hali hiyo inaonesha mwitikio mkubwa wa maombi ya ajira huku kibali kilichotolewa kwa kada mbalimbali za afya ni 7,612 huku walimu ni 9,800.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini wa ofisi hiyo, Nteghenjwa Hosseah, kwa sasa mfumo wa ajira unafanya kazi vizuri kwa kasi ya kutosha na hadi Aprili 25, mwaka 2022 saa nne usiku waombaji wa kada ya ualimu walikuwa 69,813 na kada ya Afya ni 13,683.

"Jumla ya waombaji wote ni 83,514. Waombaji wote hawa wameomba kupitia mfumo ajira.tamisemi.go.tz kwa muda wa siku tano tu, hivyo ni takribani waombaji 16,703 huwasilisha maombi kwa siku, tangazo la ajira lilitolewa Aprili 20, mwaka 2022 na mwisho wa kuomba ni Mei 4, mwaka 2022," alisema.

Hata hivyo, alisema waombaji ambao bado wanapata tatizo la kimfumo waangalie zaidi mtandao wanaotumia, eneo walipo na taarifa wanazoingiza kwenye mfumo.

Kuhusu kigezo cha mwaka kwa ajira za ualimu kuanzia mwaka 2015 hadi 2021, alifafanua; "wahitimu wa miaka ya nyuma wengi waliajiriwa moja kwa moja serikalini na wale waliokuwa wamebakia na wana sifa waliajiriwa kwenye ajira zilizotangazwa mwaka 2018 hadi 2021 hivyo kwa sasa tunaendelea na wahitimu ambao walianza na mfumo wa kutoajiriwa moja kwa moja serikalini ambao ulianza kufanya kazi mwaka 2015."

Akizungumzia kugonga muhuri vyeti vya kitaaluma, alisema sio kigezo muhimu katika uombaji wa ajira hizo na mwombaji anaweza kuomba bila kugonga muhuri kwa Mwanasheria na maombi yatapokelewa na kufanyiwa kazi.

"Lugha inayotumika kuandika barua ya maombi, waombaji wanaweza kutumia lugha yeyote (Kiswahili au Kiingereza) kutuma maombi yao, kwa wasifu hakuna sehemu ya kuweka wasifu kwenye mfumo wa ajira hivyo waombaji wote wafuate maelekezo yaliyopo kwenye mfumo," alisema.

Alisema waombaji wote wanatakiwa kujisajili na kufungua akaunti mpya hata kama alishawahi kuwa na akaunti aliyotumia kuomba ajira zilizopita ndiyo aendelee na maombi ya ajira za mwaka 2022.

"Kwa sasa mikoa na halmashauri zote zenye uhitaji wa watumishi wa kada ya ualimu na afya zinaonekana kwenye mfumo: Kwa wale waliokutana na changamoto hii hapo awali wanaweza kujaza tena kipengele hiki. Kwa sasa kozi zote za vyuo vilivyosajiliwa TCU na NACTE zimewekwa kwenye mfumo kama utaendelea kukutana na changamoto hii wasiliana na kituo cha huduma kwa mteja kwa msaada zaidi," alisema.

Alisema kwa mujibu wa kibali cha ajira, masomo yote yaliyopata kibali yameingizwa kwenye mfumo kama mtu atakuwa haoni somo la pili la kufundishia itakuwa somo hilo halipo kwenye kibali cha ajira.


## TENDER NOTICE

Ubalozi wa kifalme wa Saudi Arabia unatangaza tenda ya kampuni ya Ulinzi inayoweza kufanya kazi nao, kila kampuni inayoomba ilete barua ya maombi ubalozini.

Mwisho wa tenda ni wiki mbili kuanzia tangazo la gazeti hili.

Kwa mawasiliano piga namba
+255222667833 / +255222668203
Ada Estate Plot No. 44 Galu Street
Email: tzemb@mofa.gov.sa

116823402



## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**REMIJO ANANIA TWEVE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari ya gari aina ya **HONDA CRV** yenye usajili namba **T135 BAC,** CHASSIS NAMBA **B20B1020531,** ENGINE NAMBA **RD11018945.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**MKB/RB/IR/78/2022**


**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO.250/2018**

**REILA YOWEN SANGA..............................MDAI**

**DHIDI YA**

**1: SAID KYANI................................................MDAIWA**
**2: YUSUPH KIBONA........................................MDAIWA**
**3: LETSHEGO BANK........................................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: SAID KYANI**

Fahamu kwamba **REILA YOWEN SANGA** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 10/05/2022 saa 2.30 asubuhi mbele ya Mh. A Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 12 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukos wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.

A. Mapunda
MWENYEKITI
14/04/2022.

CHAIRMAN
DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
MBEYA
TANZANIA

## Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together, we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2022 .

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2022 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2021 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 721.70 | 832.82 |
| 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 5,136.14 | 9,467.90 |
| 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 36,788.55 | 35,070.14 |
| 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 281.95 | 529.37 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 21.87 | 141.50 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 30,668.01 | 36,356.91 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 47,142.37 | 51,115.39 |
| 12 Mali Nyingine | 1,123.88 | 1,069.55 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 634.84 | 726.37 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **122,519.32** | **135,309.96** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 23,492.50 | 36,430.00 |
| 18 Amana za Wateja | 54,994.74 | 56,654.61 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,434.98 | 1,533.45 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 1,750.47 | 453.03 |
| 28 Madeni | - | - |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **81,672.69** | **95,071.09** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **40,846.63** | **40,238.87** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 1,391.88 | 1,279.37 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | 6,016.99 | 3,516.20 |
| 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 607.76 | 2,613.31 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,846.63** | **40,238.87** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 5,120.63 | 6,760.70 |
| 39 Mikopo Chechefu | 1,632.81 | 1,632.81 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 445.17 | 437.92 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.34% | 29.74% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 3.43% | 3.17% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 60.61% | 55.42% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.48% | 37.78% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 93.77% | 90.96% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -15.68% | 14.57% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -9.45% | 11.30% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2022 | Robo ya mwaka linganishi (mwaka uliopita) 31 Marchi 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Marchi 2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 2,498.83 | 2,344.44 | 2,498.83 | 2,344.44 |
| 2 Gharama za Riba | 860.40 | 811.16 | 860.40 | 811.16 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **1,638.42** | **1,533.28** | **1,638.42** | **1,533.28** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 7.25 | 92.33 | 7.25 | 92.33 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **120.93** | **171.32** | **120.93** | **171.32** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 61.92 | 47.83 | 61.92 | 47.83 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 59.01 | 123.49 | 59.01 | 123.49 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **844.34** | **744.48** | **844.34** | **744.48** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 366.45 | 334.61 | 366.45 | 334.61 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 5.83 | 5.18 | 5.83 | 5.18 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 472.06 | 404.69 | 472.06 | 404.69 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **907.76** | **867.78** | **907.76** | **867.78** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 300.00 | 270.00 | 300.00 | 270.00 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **607.76** | **597.78** | **607.76** | **597.78** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 19 | 18 | 19 | 18 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 19 | 18 | 19 | 18 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.89% | 2.01% | 1.89% | 2.01% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.96% | 6.29% | 5.96% | 6.29% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 47.99% | 43.68% | 47.99% | 43.68% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.53% | 5.52% | 5.53% | 5.52% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 31/03/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **32,830.00** | - | **6,129.50** | **1,279.37** | - | - | **40,238.87** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 607.76 | - | - | - | **607.76** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (112.51) | 112.51 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka wa sasa** | **32,830.00** | - | **6,624.75** | **1,391.88** | - | - | **40,846.63** |
| **Mwaka Uliopita 31/12/2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **4,754.21** | **41.35** | - | - | **37,625.56** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,613.31 | - | - | - | **2,613.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,238.02) | 1,238.02 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **32,830.00** | - | **6,129.50** | **1,279.37** | - | - | **40,238.87** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Machi 2022**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | OFISA MTENDAJI MKUU | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi..**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |
| INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |
| MWANAIDI ATHUMAN MTANDA | MKURUGENZI | (Imesainiwa) | 20-04-2022 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 MACHI 2022

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka ya sasa 31 Machi 2022 | Robo Mwaka iliopita 31 Desemba 2021 | Limbikizo la mwaka wa sasa 31 Machi 2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 31 Marchi 2021 |
|---|---|---|---|---|
| **I Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 607.76 | 620.99 | 607.76 | 597.78 |
| Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| Hasara katika mali | (310.71) | 100.65 | (310.71) | 100.56 |
| -Badiliko halisi katika Mikopo | 3,973.02 | 697.07 | 3,973.02 | 4,069.15 |
| Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Amana | (14,597.37) | 9,108.10 | (14,597.37) | (3,861.80) |
| Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 1,566.48 | (569.87) | 1,566.48 | 73.57 |
| Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (2,618.30) | 1,843.78 | (2,618.30) | 1,950.84 |
| Kodi iliyolipwa | (300.00) | (317.85) | (300.00) | (270.00) |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(11,679.12)** | **11,482.86** | **(11,679.12)** | **2,660.12** |
| **II Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | **-** | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za kudumu | 402.25 | 0.21 | 402.25 | (5.35) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (570.60) | 165.85 | (570.60) | 557.44 |
| Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(168.35)** | **166.06** | **(168.35)** | **552.10** |
| **III Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo(bainisha) | (67.56) | (65.91) | (67.56) | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(67.56)** | **(65.91)** | **(67.56)** | **-** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (11,915.02) | 11,583.01 | (11,915.02) | 3,212.21 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka/mwaka | 47,101.31 | 35,518.30 | 47,101.31 | 36,896.83 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/mwaka** | **35,186.28** | **47,101.31** | **35,186.28** | **40,109.04** |

**Canara Bank (T) Ltd**
**Head Office Dar Es Salaam Branch**
**Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania**
**E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532**
**www.canarabank.co.tz**

216824602

# Operesheni yanasa 'Panya road' waliovunja nyumba 23

**Na Romana Mallya**

KUNDI la watoto wenye umri kuanzia miaka minane hadi 12 maarufu 'panya road' wamepita nyumba kwa nyumba maeneo ya Zingiziwa kata ya Chanika, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam wakiwa na mapanga na kujeruhi kisha kupora mali na fedha.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliyasema hayo jana na kueleza kuwa tukio hilo limetokea Jumapili usiku baada ya kundi hilo kuvamia nyumba 23.

"Vitoto vidogo sitaki kuviita 'panya buku', 'panya road' vinapita kwenye nyumba za watu kuvunja vioo, kuiba kujeruhi nimeagiza Jeshi la Polisi wafanye operesheni wengi wamekamatwa.

"Niwaase wazazi, Mkuu wa wilaya ulitoa tamko mara baada ya tukio, niwaase wazazi muulize mwanao anaporudi jioni, ulikwenda kufanya kazi gani leo au anaporudi asubuhi ulikuwa wapi na nani, asije akarudi nyumbani na TV akakwambia amebeti, asije akarudi na simu akakwambia amepata kwenye promosheni mwongo."

Makalla alisema katika msako huo wamekamata simu nyingi, runinga karibu 13 na fedha 1,260,000.

"Watoto wenyewe ni wengi, operesheni iliyofanyika jana (juzi) na leo (jana) wazazi mkawatambue watoto wenu kule, wengi wamekamatwa halafu miaka minane mpaka 12 huyu si bado anasoma, wazazi muwe walinzi wa kwanza wa kuwalinda watoto," aliagiza.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wawaulize watoto wao shughuli wanazozifanya na wasipokee mali wanazokwenda nazo nyumbani.

## Miili ya vijana 9 wa Kikatoliki yaagwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MIILI tisa ya waumini wa Kanisa Katoliki mkoani Njombe waliofariki kwa ajali ya gari wilayani Wanging'ombe imeagwa jana kwa ibada iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Joseph.

Akizungumza wakati wa ibada ya mazishi jana, Mkuu wa Mawasiliano Jimbo Katoliki la Njombe, Padri Eusebius Kyando, alisema Aprili 24, Umoja wa Vijana Katoliki Jimbo la Njombe pamoja na walezi wao walikuwa wanarudi katika safari yao ya kitume walikokwenda kuwatembelea watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika kituo cha Dorothea Upendo kilichopo Ibumila Parokia ya Mtwango.

Kyando alisema saa 11 jioni katika eneo la njiapanda Igima walipata ajali na watu watatu kufariki papo hapo na wengine sita kufariki wakati wakipatiwa huduma hospitalini.

Alisema toka mwaka 2020 vijana wa Uvikanjo Parokia ya Njombe wamekuwa wakifanya kazi ya utume kwa kutembelea jumuiya ndogo ndogo na watu wenye mazingira magumu na kufanya matendo ya huruma katika vituo hivyo.

Pia, aliishukuru Serikali ya Mkoa wa Njombe kwa kuwa karibu na kanisa hilo hasa baada ya kutokea ajali hiyo na maandalizi ya ibada ya mazishi ya kuwasindikiza marehemu hao kwenye nyumba yao ya milele.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba alisema, baada ya kupata taarifa ya ajali hiyo alivielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kufika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Njombe na ya Halmashauri ya mji Njombe kwa ajili ya kuangalia majeruhi pamoja na marehemu waliotokana na ajali hiyo.

Askofu wa Jimbo la Mbinga anayesimamia Jimbo Katoliki la Njombe, John Ndimbo, alishukuru Serikali ya Mkoa wa Njombe kwa kushiriki kwa ukaribu tangu tukio hilo litokee juzi.

Alitoa pole kwa familia zilizofikwa na msiba huo mzito kwa kuupokea kwa imani na uvumilivu mkubwa na pia kushiriki toka taarifa za ajali zilipotolewa mpaka sasa.

Baadhi ya waumini walioshiriki ibada hiyo wakiwamo Ditram Mbunda na Ng'amilo walisema msiba huo umewagusa kwa kiasi kikubwa na kuwaumiza kwa kuwa ni tukio kubwa kutokea hivi karibuni mkoani hapo.


BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB)

MKUTANO WA MASHAURIANO NA WADAU WA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA 2022

*"Umuhimu na Mchango wa Makandarasi katika uchumi wa Tanzania".*

Dodoma; Tarehe 12 - 13 Mei 2022, Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre

Bodi ya Usajili wa Makandarasi **(CRB)** inapenda kuwataarifu **Makandarasi** na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wakiwemo **Waajiri, Wataalam Washauri** (Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi) na wataalam mbalimbali katika sekta ya ujenzi kuwa imeandaa mkutano wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi utakaofanyika **Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma.tarehe 12 - 13 Mei 2022** kuanzia **saa 2.00 asubuhi**. Kaulimbiu ya mkutano ni: *"Umuhimu na mchango wa Makandarasi katika uchumi wa Tanzania"*. Mada zifuatazo zitajadiliwa:-

- Mchango wa makandarasi katika uchumi wa Tanzania
- Changamoto zinazoathiri mchango wa Makandarasi katika uchumi wa Tanzania – Mkandarasi
- Masuala muhimu ya kodi ya kuzingatiwa na Makandarasi ili kuboresha mchango wao katika uchumi wa Taifa
- Fursa katika sheria na kanuni za manunuzi ya umma kuwezesha mchango wa Makandarasi wa ndani katika uchumi wa Tanzania
- Utatuzi wa migogoro katika ununuzi wa umma

Mkutano pia utaambatana na Maonesho ya Teknolojia, Huduma na Vifaa vya Ujenzi.

| | |
|---|---|
| **Walengwa** | Makandarasi, Wataalam washauri; Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Wahandisi, Wataalam wanaoshabihiana nao, Waajiri, Watunga sera za uwezeshaji wananchi kiuchumi na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wanaalikwa kushiriki. |
| **Ada ya Ushiriki** | Ada ya ushiriki ni **TZS 50,000/=** kwa Makandarasi na **TZS 100,000**/= kwa Wadau wengine. Ada itagharamia mahitaji ya mkutano kama ukumbi, chakula cha mchana na vinywaji.<br><br>Ada ya ushiriki italipwa kwa utaratibu ufuatao:-<br>Malipo ya ada ya ushiriki yafanywe benki ya **CRDB Plc** au **NBC ltd**. au **NMB Plc** kwa jina la **CONTRACTORS REGISTRATION BOARD** pia kwa kupitia mitandao ya simu kwa kutumia **"Control Numbers** kama ifuatavyo:-<br>**Makandarasi**<br>"Control Number" **995740048661**<br>**Wadau wengine**<br>"Control Number" **995740048660**<br>Hakikisha **namba ya simu ya mshiriki** imeoneshwa katika karatasi ya malipo ya benki. |
| **Maonesho (Exhibitions)** | Bodi inayaalika makampuni na watu binafsi kushiriki kwa kuonesha teknolojia, huduma, bidhaa, vifaa na zana za Ujenzi kwa lengo la kuzitangaza kwa wadau wa sekta ya ujenzi. Watakaopenda kushiriki maonesho hayo wawasiliane na **Ndugu Alois Manamba** kwa simu namba **0715809473** au kwa barua pepe kwa anwani almanamba@gmail.com au crbhq@crbtz.org au **Eng. Awadh** kwa namba ya simu **0713336987** au kwa barua pepe **aaawadh@yahoo.com**. |
| **Jinsi ya Kujisajili** | Washiriki wathibitishe kuhudhuria mkutano kwa kulipa ada ya ushiriki angalau siku kumi (10) kabla ya tarehe ya mkutano na kutuma majina na mawasiliano yao katika ofisi yoyote ya **CRB** nchini. **Washiriki wanahimizwa kujisajili mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.** |
| **Mafunzo endelevu (PDU)** | Washiriki ambao ni wataalam wa fani za ujenzi watatuzwa alama za mafunzo endelevu **(AQRB-16 CPDs, ERB-13 PDUs)**, zitakazotolewa na Bodi zao za usajili. |

**Kwa taarifa zaidi fanya mawasiliano kama ifuatavyo:-**

**CRB Makao makuu**, S.L.P 96 Dodoma Simu 026 2962403/4, Tovuti: www.crb.go.tz,
Barua pepe: crbhq@crb.go.tz

**CRB Kanda ya Mashariki**, S.L.P 33621 Dar es Salaam Simu 022 2771877, Barua pepe: crbez@crbtz.org

**CRB Kanda ya Ziwa**, S.L.P 2815 Mwanza Simu 028 2500218, Barua pepe: crblz@crbtz.org

**CRB Kanda ya Kusini**, S.L.P 1690 Mbeya Simu 025 2502480, Barua pepe: crbsz@crbtz.org

**CRB Kanda ya Kaskazini**, S.L.P 16795 Arusha Simu 027 2547107, Barua pepe: crbnz@crbtz.org

**CRB Kanda ya Kati**, S.L.P 2618 Simu 026 2966040, Barua pepe: crbcz@crbtz.org

216823602


## CAG akuta mabilioni fedha za mirathi BoT

**Na Sanula Athanas,** MBEYA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini kuwapo mabilioni ya shilingi kwenye akaunti maalum Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliyofunguliwa kwa ajili ya kuhifadhi fedha za mirathi huku akikosa rejista ya wanaostahili kulipwa fedha hizo.

CAG Charles Kichere, amebainisha hayo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12, mwaka huu.

Anafafanua kuwa Kanuni ya 131(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (Toleo la mwaka 2004), inahitaji kiasi kilichopo kwenye akaunti moja moja za amana mwishoni mwa mwaka wa fedha kuorodheshwa na kufanyiwa usuluhisho na salio lililopo kwenye akaunti husika za udhibiti.

"Wakati wa ukaguzi wa Mahakama, nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, mahakama kama msimamizi wa mirathi, ilikuwa na jumla wa Sh. 26,656,717,909.04 (Sh. bilioni 26.657) katika akaunti ya mirathi iliyopo Benki Kuu.

"Hata hivyo, hakukuwa na rejista inayoonyesha orodha ya wanufaika wa kiasi hicho; hivyo usuluhishi wa rejista na akaunti ya benki haukuweza kufanyika kama inavyotakiwa na kanuni za fedha.

"Matokeo yake, ilikuwa vigumu kujua wanufaika wa fedha hizo za mirathi. Kutokana na hilo, ni maoni yangu kwamba menejimenti imekuwa na upungufu katika usimamizi wa fedha za mirathi zilizo chini ya uangalizi wa mahakama.

"Niligundua kuwa ukosefu wa sheria na kanuni sahihi za usimamizi wa fedha hizo ni sababu ya upungufu huu. Kwa kukosekana kwa usimamizi sahihi wa fedha hizi za mirathi, kunaziweka fedha hizo katika hatari za kutumiwa vibaya au akaunti hiyo kutumika kufanya miamala isiyoendana na lengo na madhumuni husika.

"Ninashauri Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuhakikisha kwamba; kuna sheria na miongozo ya kifedha itakayoelekeza usimamizi wa fedha za mirathi na kuanzisha rejista mtandao ambayo itasajili wanufaika wote wa fedha hizo," CAG anawasilisha hoja yake.

### UHABA WA WATUMISHI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pia anasema kuwa amebaini upungufu wa watumishi 33,145 katika wizara, idara, wakala za serikali, taasisi zingine na sekretarieti za mikoa.

Anasema idadi hiyo ni sawa na asilimia 42 ya mahitaji ya watumishi 57,313 yaliyobainishwa na taasisi za umma.

### MAKOSA KUKOKOTOA MAFAO

CAG pia anasema kuwa atika ukaguzi wake wa majalada ya mafao 1,880 aliyoyaidhinisha kwa malipo, alibaini majalada 314 (16.7%) yalikokotolewa kimakosa.

Anasema makosa hayo yanatokana na kipindi kisicho sahihi cha utumishi, mishahara isiyo sahihi iliyotumika kukokotoa mafao, michango ya watumishi isiyo sahihi na makosa ya majumuifu.

"Hata hivyo, makosa hayo yalirekebishwa na majalada hayo niliyaidhinisha kwa malipo. Kati ya majalada 314 yaliyokokotolewa kimakosa, majalada 208 (66.2%) yalikokotolewa zaidi ya kiwango stahiki kwa Sh. milioni 489.67 na majalada 106 (33.8%) yalikokotolewa kwa kiwango pungufu kwa Sh. milioni 274.15.

"Naishauri serikali iwe na utaratibu ambao utahakikisha mafao ya watumishi waliomaliza muda kazini yanakokotolewa kwa usahihi kabla ya kuwasilishwa kwa ukaguzi wa awali ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa mafao yao kwa wakati. Hii itasaidia kupunguza hatari ya upotezaji wa fedha za serikali endapo madai yatakayozidi kiwango stahiki hayatabainika.

"Vilevile, itasaidia kuwalinda wastaafu wasilipwe pungufu ya stahiki zao kutokana na mapunjo katika mafao yao," CAG anawasilisha hoja yake.

### WASUBIRI MAFAO MIAKA 28

CAG pia anabainisha kuwa katika ukaguzi wa mwaka 2020/21, alibaini ucheleweshwaji kwenye uandaaji na uwasilishwaji wa majalada ya mafao 571 kwa ajili ya ukaguzi wa awali kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 28.

"Ucheleweshwaji huo unaathiri hali ya maisha ya wastaafu, kwani wengi wao hutegemea mafao ya kustaafu kama pato la kuendesha maisha yao baada ya kumaliza utumishi wa umma.

"Ucheleweshaji uliokithiri wa kurudisha majalada yaliyohojiwa pia unasababisha kuchelewa kwa malipo ya mafao na kuathiri hali ya maisha ya wastaafu," CAG anatoa angalizo.

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

## TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 2,911 | 3,289 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,287 | 7,028 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,436 | 43,178 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 114,554 | 111,923 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 129,669 | 133,954 |
| | - | - |
| 12 Mali Nyingine | 25,189 | 31,238 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,342 | 3,178 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **335,386** | **334,788** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 69,416 | 106,867 |
| 18 Amana za Wateja | 132,293 | 114,136 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 Dhima Nyingine | 6,352 | 2,815 |
| 28 Madeni | 100,354 | 74,640 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **308,414** | **298,459** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **26,972** | **36,329** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 105,114 | 105,114 |
| 32 Hisa za Upendeleo | 17,840 | 17,840 |
| 33 Akiba ya Mtaji | - | - |
| 34 Hifadhi ya hatari ya benki kuu | 2,163 | 1,716 |
| 35 Mapato Yaliyobakizwa | (99,134) | (89,329) |
| 36 Akaunti Nyingine za Mtaji | 989 | 989 |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **26,972** | **36,329** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 674 | 2,866 |
| 39 Mikopo Chechefu | 16,315 | 19,585 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,862 | 15,128 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.04% | 10.85% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11.53% | 13.14% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 70.17% | 67.46% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 42.20% | 44.53% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 49.00% | 47.28% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 15.91% | 18.11% |
| (vii Ongezeko la Mali | 0.18% | 8.28% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 40,620 | 42,736 |
| 2 Gharama za Riba | (20,403) | (19,652) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **20,217** | **23,084** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (1,278) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **4,926** | **4,344** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 931 | (321) |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 3,995 | 4,665 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(34,221)** | **(31,803)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (10,309) | (10,355) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | (1,569) | (1,077) |
| 7.3 Gharama Nyingine | (22,343) | (20,371) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(9,078)** | **(5,653)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (279) | (145) |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(9,357)** | **(5,799)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | 76 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(9,357)** | **(5,723)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 167 | 154 |
| 14 Mapato kwa Hisa | -89% | -55% |
| 15 | 0% | 0% |
| 16 Idadi ya Matawi | 6 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.71% | -1.69% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -33.66% | -15.56% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -136.11% | -115.95% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.75% | 2.00% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-21 | Mwaka uliopita 31-Dec-20 |
|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (9,078) | (5,653) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 3,718 | 5,380 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 4,285 | (8,018) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (19,295) | 27,921 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (258) | (10,127) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,537 | (1,541) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 6,049 | (4,234) |
| - Kodi Iliyolipwa | (279) | (135) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(11,321)** | **3,593** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (6,881) | (641) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(6,881)** | **(641)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 25,713 | 5,088 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **25,713** | **5,088** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 7,511 | 8,040 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 122,240 | 114,200 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **129,751** | **122,240** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2021** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (89,329) | 1,716 | - | 989 | 36,329 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (9,357) | - | - | - | (9,357) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (447) | 447 | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | - | - | (9,804) | 447 | - | - | (9,357) |
| | | | | | | | - |
| **Mwaka Uliopita 2020** | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (80,526) | 130 | - | 1,065 | 43,623 |
| Athari za urekebishaji wa makosa | - | - | (1,420) | - | - | - | (1,420) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (5,799) | - | - | - | (5,799) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | (76) | (76) |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,586) | 1,586 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (89,329) | 1,716 | - | 989 | 36,329 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na Ernst & Young, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

Taarifa hizi za fedha ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya tarehe 21 April 2022

I. John
**(Mkurugenzi mtendaji)** **Imesainiwa tarehe 21 April 2022**

Mr. P. Ishengoma
**(Mkurugenzi)** **Imesainiwa tarehe 21 April 2022**

XXXXXXXX

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole TRA kwa kutoa msamaha huu

**JUZI** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitangaza msamaha wa adhabu na riba ya kodi kwa vyombo vya moto vilivyoingizwa nchini bila kufuata taratibu za forodha vikiwamo vilivyoingizwa kwa njia zisizo rasmi.

Pia, vilivyokusudiwa kwenda nchi jirani na vikaingizwa nchini kinyume cha taratibu vilivyoingizwa nchini kwa muda na kuzidisha muda wa kukaa nchini na vilivyotumia msamaha wa kodi kinyume cha sheria au kubadilisha umiliki bila kufuata utaratibu.

TRA ilisema msamaha huo unatolewa kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 70 kifungu kidogo cha pili cha sheria ya usimamizi wa kodi ya mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marekebisho na sheria ya fedha ya mwaka 2021 pamoja na kifungu cha 249 cha sheria ya usimamizi wa uhuru wa forodha ya Jumuiya Afrika Mashariki ya 2004 ambazo zinampa kamishna wa TRA mamlaka ya kusamehe riba na adhabu.

Aidha, ilibainisha kuwa msamaha huo unatolewa kuanzia jana hadi Juni 30, mwaka huu, ukiwa na lengo la kutoa unafuu kwa wamiliki wa vyombo vya moto vyenye madeni ya kodi na adhabu, ili kulipa kodi waliyokadiriwa tu bila adhabu na riba.

Mamlaka hiyo ilisema msamaha huo umelenga kujenga ushirikiano na uhusiano mwema kati ya TRA na walipakodi husika, kuwapa motisha ya kulipa kodi kwa hiari na wakati pamoja na kuweka kumbukumbu au taarifa sahihi za umiliki wa vyombo hivyo.

Tunaipongeza TRA kwa hatua hii kwa kuwa tunaamini inakwenda kuleta mabadiliko na kwamba yenyewe itapata kodi yake ambayo itaelekezwa kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali.

Lakini itapunguza au kuondoa kabisa msongamano wa magari yaliyokuwa yamekamatwa kwenye maeneo mbalimbali ya bandari, maana yake hata wenye jukumu ya kulinda watapunguziwa mzigo kwa kiasi kikubwa.

Tunaamini utasaidia wananchi kupata vyombo vyao vya usafiri ambavyo watavitumia nchini au nchi walizokuwa wanapeleka, maana yake yalibaki na huenda mengine yaliharibika au kutolewa vifaa kabla ya kuwafikia wahusika.

Tunawasihi wafanyabiashara na wote waliokwama kutoa magari yao kwa sababu ya riba na adhabu mbalimbali,kutumia vyema muda uliotolewa kwa kuchukua mali zao kuliko kuacha kabisa kwa kuwa ndiyo wakati mwafaka.

Hii ni motisha nzuri inayopaswa kuigwa,kwa kuwa ili nchi iendelee inahitaji kodi na lazima ipatikane kutoka kwa wananchi wa nchi yake,pale ambako inaonekana kuna linaloweza kufanyika kurahisisha kodi kulipwa ni jambo jema kama TRA walivyofanya.

Tunaisihi TRA kuangalia maeneo mengine ambayo wanaweza kukusanya kodi ya serikali kwa urahisi kwa kutoa motisha kama walivyofanya kwa wenye magari haya.

Lakini elimu kwa walipa kodi na kujenga mazingira rafiki ili walipe kodi halisia kwa hiyari ni muhimu sana,kwa maendeleo ya nchi,kwa kuwa tunaamini wanaolipa kwa hiyari ni wenye kuipenda nchi yao.

Tunaamini wananchi wakielimishwa na kuona kodi zao zinatumika vizuri na kwamba zinaleta mabadiliko kwenye maisha yao,watalipa kwa hiyari na watafurahia kulipa.

Nchi zilizoendelea mtu kukwepa kodi ni kosa kubwa la jinai, na hatua kubwa huchukuliwa haraka kwa wahusika bila kujali umaarufu wala nafasi ya mhusika katika jamii.


Kwa nchi za Afrika,wakati mwingine ni kawaida kusikia mfanyabiashara au mtu maarufu fulani amekwepa kodi, na bado asijitokeze mbele ya umma kuonyesha anajutia na kulipa fedha ya umma.

Ni lazima kujenga nidhamu ya watu kuipenda nchi yao na kuona kulipa kodi ni jukumu la lazima kwake,hapaswi kukwepa kwa namna yoyote bali ajitokeze mbele ya umma kujisifu alivyolipa kodi nzuri kwa nchi yake.

Naamini kila Mtanzania akilipa kodi kwa hiyari tutakuwa na fedha nyingi ambazo zikielekezwa kwenye matumizi sahihi ya kuhudumia wananchi kwenye mambo yanayowagusa moja kwa moja,zitasaidia kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Miaka 58 dira iwe wosia wa Nyerere kwa Muungano

Na Gaudensia Mngumi

**JUBILII** ya miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, imekamilika. Ni hatua inayoashiria kuelekea kwenye miaka na miongo mingi zaidi.

Ni takriban miaka 60 sasa Muungano umeishi ukilelewa na kutunzwa na viongozi ambao kila wakati wameondoa na kupunguza kero zinazoibuka.

Pongezi kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Dk. Hussein Ali Mwinyi na viongozi wa Tanzania Bara na Zanzibar ambao wamekuwa waamini na watetezi wakubwa wa Muungano, tangu 1964.

Jubilii hii ni chachu ya kuwahimiza viongozi washindane kujadili udhaifu au changamoto kwa sababu, Muungano upo na umeishi.

Pamoja na hayo, ukweli lazima tuseme kuwa miaka 58 ya Muungano ni mwongozo unaoonyesha kuwa hakuna haja ya kurudi nyuma bali cha kushughulikia ni kero za Muungano ili uwanufaishe Watanzania Bara na Wazanzibari.

Awamu ya sita iendelee kutatua kero kwa kuangalia Watanganyika wanataka au wanalalamikia nini kadhalika Wazanzibari wanahitaji nini ili kuwe na tija zaidi.

Muungano unakubalika na unapendwa na Watanzania wa Bara na Zanzibar na hilo limethibitika kwenye Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Warioba, wengi walilalamikia au kuzungumzia kero za Muungano lakini si kupinga uwepo wa Muungano. Wanaonyesha kuwa wanaupenda.

Huo ni udhihirisho kuwa wengi wanakubaliana na Muungano na wanataka uishi zaidi ufikie hata mwisho wa dahari.

Muungano ni dira inayoiongoza katiba kwani ndiyo unaowaelekeza Watanzania Bara na Visiwani jinsi ya kuendeleza na kuongoza Serikali za Zanzibar na Tanganyika.

Watanzania wa leo wana jukumu la kuendeleza Muungano wakikumbuka kuwa viongozi waasisi

Abeid Karume na Mwalimu Nyerere walisaini mikataba, walitoa maagizo ya kimaandishi walizindua miradi, wakatangaza mikakati hivyo, umma uliopo uendelee kutimiza malengo hayo.

Wakati wa kutafakari na kusherehekea miaka 58 ya Muungano ni vyema kukumbuka wosia ambao Mwalimu Nyerere alisema :

"Atakayevunja Muungano hatabaki salama" na kueleza kuwa Muungano umesaidia kudumisha amani ya Zanzibar, Tanganyika na Pemba.

Hata leo inawezekana Waunguja na Wapemba hawakubaliani katika mambo mengi lakini kwa kuwepo Muungano wanaishi kwa amani bila uhasama, hilo ni jambo jema ambalo Watanzania wanatakiwa kulienzi.

Masuala ya kutaka serikali tatu au mbili huenda yakaendelea kujadilika lakini pengine kikubwa kinachohitajika zaidi ni kuwa na katiba mpya ya kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini na kuwa na maisha bora zaidi.

Jambo la msingi ni kuandika katiba ya kuwasaidia wananchi siyo kuendelea kutaka serikali nyingi ili kuwa na eneo kubwa la utawala na gharama kubwa ya kuendesha serikali kwa kugawa madaraka badala ya kuondoa umaskini unaowakera watoto, vijana na wazee wa Tanzania Bara, Unguja na Pemba, usipewe nafasi.

Marais Samia na Mwinyi kama watangulizi wao wamesimama muda wote kutetea .

Pengine ni kutokana na Mama kuwa na msimamo alioupata kwa muda mrefu kutokana na kuhudumu na kuulea akiwa Waziri Ofisi ya Muungano na pia Makamu wa Rais akiwa na jukumu la kushughulikia masuala ya Muungano.

Ni jambo la kujivunia kuona kuwa Tanzania ina viongozi wanaoendelea kuvaa viatu vya kuutetea Muungano kama walivyofanya Abeid Amani Karume, Mwalimu Julius Nyerere, Aboud Jumbe, Thabiti Kombo na Ben Mkapa.

Juhudi za Serikali ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar, zinaonyesha kuwa licha ya kizazi kinachofahamu habari za Muungano na kutetea, kilichozaliwa na kulelewa na waasisi Nyerere na Karume kuelekea kutoweka, jitihada zinafanywa kuwahimiza vijana kuupenda na kuuenzi Muungano.

Hivyo, baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kudumu miaka 58, ni wakati wa kupunguza kero ili kuudumisha zaidi.

# Watoto mil. 10 nchini kesho kupata chanjo polio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPENI ya chanjo ya matone ya polio, inatarajiwa kuanza kutolewa kesho nchi nzima kwa watoto zaidi ya milioni 10 walio chini ya umri wa miaka mitano.

Ofisa Programu kutoka Wizara ya Afya katika Mpango wa Taifa wa chanjo, Lotalia Gadau, alitoa kauli hiyo kwenye semina ya Waharíri wa vyombo mbalimbali vya habari jijini hapa.

Alisema kampeni hiyo itafanyika kwa awamu nne, ya kwanza imefanyika katika mikoa minne inayopakana na Malawi ambayo ni Njombe, Mbeya, Ruvuma na Songwe.

Pia, alisema awamu ya pili itafanyika kwa siku nne kuanzia kesho hadi Mei mosi na itakuwa nyumba kwa nyumba.

Alibainisha kuwa dozi za chanjo hiyo zilizopo nchini ni zaidi ya milioni 13.32.

"Hii chanjo itatolewa kwa watoto wote walio chini ya umri wa miaka mitano bila kujali hali zao za chanjo za awali, hii ni kampeni maalum hata kama amepata chanjo jana, leo tunampatia hii, ni ya kuendelea kuongeza kinga mwilini, hata kama kesho anaratiba ya chanjo aende kuchanja kama kawaida," alisema.

Ofisa huyo alisema mara ya mwisho kupata mgonjwa wa polio nchini ilikuwa 1996 mkoani Mtwara na mwaka 2015 Tanzania ilipata cheti cha kuonesha hakuna polio kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO).

"Kutokana na Malawi kupata hili janga inatupa wasiwasi kuwa cheti chetu huenda tutanyang'anywa endapo hatutafanya mikakati ya kukabiliana na huu ugonjwa, ndiyo maana tunaendelea na jitihada kuhakikisha polio haiingii nchini, tumeimarisha utoaji chanjo ndiyo maana tangu mwaka 1996 hatujapata kesi," alisema.

Alitoa wito kwa vyombo vya habari nchini kushiriki ipasavyo kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa chanjo hiyo.

"Kwa awamu ya kwanza tumevuka lengo tuliloweka tulipata idadi kubwa. Kutakuwapo na timu za uchanjaji na uhamasishaji itakuwa nyumba kwa nyumba na chanjo hii haina kitu nyuma yake bali inalenga kumfikia kila mtoto popote alipo hata kwenye nyumba za ibada," alisema.

Kwa upande wake, Mratibu wa kampeni ya kutokomeza ugonjwa wa Polio Tanzania, Dk. Anthony Kazoka, alisema polio ni ugonjwa wa pili ambao wanatakiwa kuutokomeza duniani baada ya ndui kutokomezwa.

Alisema mkakati wa kutokomeza umefikia asilimia 98 na bado nchi mbili duniani zina ugonjwa huo wa polio ambazo ni Pakistan na Afghanistan.

"Hakuna madhara ya kuongeza chanjo kwa kuwa inaongeza kinga, watapewa chanjo bila kuangalia hali zao za chanjo za awali, kwa mtoto aliyefikiwa na kupata chanjo kutakuwa na alama maalum kwa mtoto na nyumba anayoishi mtoto," alisema.

## Makalla akemea wizi miundombinu ya maji

**Na Joseph Mwendapole**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amekemea wizi wa miundombinu ya maji ikiwemo mabomba na mita za maji unaoendelea na kuwataka wananchi kushirikiana na Serikali katika kudhibiti wizi huo.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya mradi wa maji Pugu - Gongo la Mboto hususani kwa wananchi walioungan-ishwa kupitia mradi huo uliotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Alisema wizi wa mabomba na mita za maji umekithiri na kusababisha usumbufu kwa wateja pamoja na kuleta hasara kwa Serikali jambo linalorudisha nyuma nia njema ya Serikali ya kuwaunganishia maji wananchi wake.

"Serikali inatumia fedha nyingi kuhakikisha huduma ya maji inapatikana kwa wananchi na hii ndio kazi inayofanywa na DAWASA, hivyo si vyema kwa mwananchi kuhujumu miundombinu ya maji," alisema Makalla.

Makalla aliipongeza DAWASA kwa kutekeleza miradi mikubwa kwa kutumia fedha za ndani pamoja na ubunifu wa kuwaunganishia wananchi maji kwa mkopo. Mbali na hilo, Makala alipongeza uamuzi wa kuhakikisha maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam yanapata huduma ya majisafi na salama wakati wote.

"Miradi yote ya maji inayotekelezwa pembezoni mwa mji ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ili kuhakikisha huduma ya majisafi inawafikia wananchi wote na kwa kweli nawapongeza DAWASA kwa kazi nzuri wanayoifanya," alisema na kuongeza.

"Nimepita mtaani kwenye nyumba za wateja na nimeona maji yakitoka tena kwa msukumo mkubwa, niwapongeze sana DAWASA kwa kazi nzuri mnayoifanya," alieleza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema mradi wa Pugu Gongo la Mboto umetekelezwa kwa kutumia shilingi bilioni 7.3 ambazo ni fedha za ndani za Mamlaka.

Alisema mradi umejenga tenki la maji lenye ujazo wa lita milioni 2 na unahudumia wakazi 450,000 wa Kata ya Pugu, Gongo la Mboto, Majohe, Bangulo, Ukonga - Airwing, Kigogo, Buyuni, Chanika, Pugu - Machimbo na Kinyerezi.

Mwanahamisi Kibuba, ambaye ni mkazi wa Kata ya Pugu - mpakani, aliishukuru DAWASA kwa kuleta maji kwenye makazi yake na kumuondolea kero ya kutumia maji ya kisima ambayo hayakua masafi.

Aliongeza kuwa maji ya kisima hua sio masafi na hayafai kwa kunywa, pia wakati mwingine hua yanakauka, nimefurahi sana kupata majisafi kutoka DAWASA. Naye mkazi wa Pugu Kajiungeni, Rachel Clement, alisema alikua anatumia fedha nyingi kwa siku kununua maji ya madumu na kumsababishia usumbufu mwingi.

"Nashukuru kwa sasa nimepata majisafi kutoka DAWASA na hivyo imesaidia kupunguza matumizi ya fedha," alisema.




MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MSAMAHA WA RIBA NA ADHABU KWA WAMILIKI WA VYOMBO VYA MOTO VILIVYOINGIZWA NCHINI KINYUME CHA SHERIA

**Dar es Salaam, 25 Aprili, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inautaarifu umma kuwa, imetoa msamaha wa adhabu na riba ya kodi kwa vyombo vya moto vilivyoingizwa nchini bila kufuata taratibu za forodha.

Vyombo hivyo vinahusisha vile vilivyoingizwa kwa njia zisizo rasmi, vilivyokusudiwa kwenda nchi jirani lakini vikaingizwa nchini kinyume na taratibu, vilivyoingizwa nchini kwa muda na kuzidisha muda wa kukaa nchini (Temporary importation) na vilivyotumia msamaha wa kodi kinyume na sheria au kubadilishwa umiliki bila kufuata taratibu.

Msamaha huu unatolewa kwa mujibu wa kifungu cha sheria namba 70 (2) cha Sheria ya usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 pamoja na kifungu cha 249 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambazo zinampa Kamishna Mkuu wa TRA mamlaka ya kusamehe riba na adhabu.

Msamaha huu unatolewa kuanzia leo hadi **Juni 30, 2022** ukiwa na lengo la **kutoa unafuu kwa wamiliki wa vyombo hivyo vya moto vyenye madeni ya kodi na adhabu, kulipa kodi waliyokadiriwa tu bila adhabu na riba.**

Vilevile, msamaha huu umelenga kujenga ushirikiano na uhusiano mwema kati ya TRA na walipakodi hao, kuwapa motisha ya kulipa kodi kwa hiari na wakati pamoja na kuweka kumbukumbu au taarifa sahihi za umiliki wa vyombo hivyo.

Kwa taarifa hii, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatoa wito kwa wamiliki wote wa vyombo hivyo vya moto kujitokeza ndani ya muda wa msamaha uliotolewa na Kamishna Mkuu **ili waweze kulipa kodi halisi inayodaiwa** na hatimaye kukomboa vyombo vyao.

Kwa maelezo zaidi juu ya msamaha huu, tafadhali tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu yako au piga simu bure namba **0800 78 00 78 au 0800 75 00 75** au unaweza kutuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp namba **0744 23 33 33** au wasiliana na TRA kwa baruapepe **huduma@tra.go.tz**.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

216825402

# Walalamikia harufu ya funza dampo Pugu

**Na Romana Mallya**

DAMPO la Pugu Kinyamwezi lililopo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Ilala limegeuka kuwa kero kwa wananchi wanaolizunguka kutokana na harufu, utiririshaji wa maji taka kwenye makazi ya watu na kutapakaa kwa funza.

Diwani Kata ya Pugu, Imelda Samjela, akizungumza juzi mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, baada ya kutembelea eneo hilo alitaja matatizo makubwa wanayopitia ikiwemo maji taka yanayotoka kwenye dampo hilo kwenda kwenye makazi ya wananchi.

"Matatizo makubwa mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ni mifereji, barabara na mlima wa takataka kama mlima Kilimanjaro, maji unayoona yanatiririka yanazunguka dampo yanatoka nje na kwenda kuwa mafuriko kwa wananchi," alisimulia.

Diwani huyo alimweleza Mkuu wa Mkoa kuwa, eneo hilo kumejengwa daraja ambalo miundombinu yake siyo mizuri na kusababisha mvua zinaponyesha maji yanafurika na kusambaa sehemu nyingine na kuingia kwa wananchi.

Pia, alisema eneo la katikati kuna mfereji ambao unatakiwa kuwekewa karavati kubwa ili kuwawezesha wanafunzi wanaopita hapo kwenda shule wasikanyage maji taka.

Matatizo mengine aliyataja diwani huyo kuwa ni jirani ya dampo hilo kumejengwa Zahanati, ambayo kuna wakati inzi huwa wengi hata mtu anashindwa kuzungumza wasiingie mdomoni.

Kutokana na dampo hilo kuzidiwa baada ya taka za mkoa mzima kupelekwa huko, diwani huyo alimuomba Makalla ikiwezekana kila halmashauri iwe na dampo lake.

"Bajeti ya mwaka 2022/23 tumetenga Sh. milioni 300 haitoshi hata kwa kitu chochote ndani ya dampo hili, tunashukuru umekuja kipindi cha mvua umejionea mwenyewe.

"Tungeongezewa angalau Sh. bilioni moja ili kupunguza matatizo, fedha zijenge barabara na kuisogeza hii milima iliyojaa na kuweka mitaro ili gari zinazoleta taka ziende eneo la ndani ambapo ukivuka kilima hiki lipo eneo kubwa huko, hata mitambo haitoshi."

Alisema wakati wa kampeni 2020 Rais wa awamu ya Tano, John Magufuli (Hayati) alivyozindua soko la Kisutu aliahidi kuwapatia Sh. bilioni 150 kwa ajili ya ukarabati wa dampo hilo na kumuomba Mkuu wa Mkoa amuombe, Rais Samia Suluhu Hassan.

Akijibu hoja hizo, Mkuu wa Mkoa, Amos Makalla alisema amezipokea baada ya kwenda hapo kujiridhisha kero zilizopo.

"Kuona ni kuamini, unaweza kukaa ofisini ukawa unasimuliwa mambo ya dampo halafu siyajui, nimeona nije muda ambao kuna kero hasa mvua na matope nione mwenyewe niseme kwamba suala la Pugu Kinyamwezi, hili la dampo ni la muda mrefu miji inapangwa binadamu wanaongezeka leo tuna kampeni ya usafi imeongeza tani za takataka Dar es Salaam," alisema.

Alisema imefika wakati ambapo Pugu haiwezi kuhudumia Manispaa zote inapaswa kila moja iwe na eneo lake la kutupa takataka.

"Jambo lingine tumeanza kupata wawekezaji kwenye madampo, tumepata kampuni tatu kutoka nchi ya China, Italia na Dubai na mazungumzo yao wanataka uhakika wa takataka, tumewapa takwimu tunazalisha tani 6,000 kwa siku, wao wanataka tani 2,000 tu kwa siku ili wazalishe umeme.

# Hospitali ya Rufani Chato yaanza kutoa huduma za moyo kibingwa

**Na Daniel Limbe,** CHATO

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Chato, imeanza kutoa huduma za kibingwa za moyo ili kuwapunguzia wananchi gharama na muda wa kwenda Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam.

Mbali na huduma za kibingwa pia hospitali hiyo inatarajia kufundisha wataalamu wa fani za udaktari na uuguzi pamoja na kufanya utafiti wa magonjwa ya binadamu.

Ofisa utumishi wa hospitali hiyo, Elly Aketch, alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe, alisema wameanza kwa mafanikio kutokana na baadhi ya wagonjwa kupatiwa huduma za kibingwa na zile za kawaida, na kwamba hatua hiyo imewasaidia wananchi kutumia gharama kidogo ikilinganishwa na kwenda Taasisi ya Jakaya Kikwete.

"Tunatarajia kutoa huduma bora zaidi ikiwezekana kuzidi hata zinazotolewa pale Taasisi ya Jakaya Kikwete tunaamini hospitali hii itakuwa mkombozi kwa wananchi waliopo Kanda wa Ziwa," alisema.

Alisema licha ya ujenzi wa baadhi ya majengo ya kulaza wagonjwa kuendelea ikiwemo jengo la huduma za mama na mtoto, wanaendelea kuimarisha huduma mbalimbali.

Aketch alisema ujenzi wa hospitali hiyo umefanyika kwa awamu tatu ukitanguliwa na majengo ya wagonjwa wa nje, dharura, maabara, dawa na wagonjwa mahututi ambayo yamekamilika.

Alisema awamu ya pili ilihusisha jengo la mama na mtoto lenye vyumba 250 ambalo litachukua wagonjwa 500 kwa wakati mmoja pamoja na jengo la mionzi.

Awamu ya tatu itahusisha jengo kubwa la ghorofa tisa ambalo litakuwa na huduma mbalimbali na kwamba litaondoa uhaba wa majengo ya kutolea huduma kwa jamii.

**TANGAZO**

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

MCB BANK — BETTER TOGETHER

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Machi-2022 | Robo Mwaka iliyopita 30-Disemba-2021 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 261 | 237 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 5,384 | 7,805 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 84 | 34 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 34 | 30 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 11,996 | 1,002 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 45,114 | 44,676 |
| 12. Mali Nyingine | 3,999 | 3,576 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 977 | 829 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **67,849** | **58,189** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 48,462 | 38,720 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,458 | 541 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 1,008 | 1,700 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 19 | - |
| 27. Dhima Nyingine | 1,036 | 1,211 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **51,982** | **42,172** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,867** | **16,017** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,950) | (18,508) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (95) | (1,387) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,867** | **16,017** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 574 | 523 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (382) | 382 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 23.4% | 27.8% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.3% | 1.1% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.3% | 113.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.9% | 77.0% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 84.2% | 79.3% |
| - Ongezeko la Amana | 25.2% | 40.7% |
| - Ongezeko la Mali | 16.6% | 23.8% |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 31-Machi-2022 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Machi-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Machi-2022 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Machi-2021 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 1,753 | 1,012 | 1,753 | 1,012 |
| 2. Gharama za Riba | 664 | 343 | 664 | 343 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,089** | **669** | **1,089** | **669** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | - | - | - |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 493 | 91 | 493 | 91 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 2 | - | 2 | - |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 446 | 91 | 446 | 91 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 45 | - | 45 | - |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,677 | 1,708 | 1,677 | 1,708 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 775 | 732 | 775 | 732 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 902 | 976 | 902 | 976 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(95)** | **(948)** | **(95)** | **(948)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(95)** | **(948)** | **(95)** | **(948)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(95)** | **(948)** | **(95)** | **(948)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 59 | 54 | 59 | 54 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -2 | -15 | -2 | -15 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-0.2%* | *-2.0%* | *-0.2%* | *-2.0%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-0.6%* | *-6.0%* | *-0.6%* | *-6.0%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *106.0%* | *225.0%* | *106.0%* | *225.0%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *1.9%* | *2.0%* | *1.9%* | *2.0%* |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji tangulizi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (95) | - | (95) |
| Mengineyo | - | (55) | - | (55) |
| Salio la mwisho wa mwaka | 30,912 | (20,045) | 5,000 | 15,867 |
| **Mwaka Uliopita** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (18,508) | 5,000 | 17,404 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (1,387) | - | (1,387) |
| Salio la mwisho wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | 16,017 |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2022 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 31-Mach-2022 | Robo Mwaka iliyopita 31-Des-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mach-2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mach-2021 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (95) | (46) | (95) | (948) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 251 | 314 | 251 | 346 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (11,432) | 255 | (11,432) | (5,766) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 9,742 | (953) | 9,742 | 5,510 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 69 | 517 | 69 | (242) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (219) | (35) | (219) | (802) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | (35) | - | - |
| - Mengineyo | - | (333) | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,685)** | **(316)** | **(1,685)** | **(1,902)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (197) | (67) | (197) | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(197)** | **(67)** | **(197)** | **-** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | 262 | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **262** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,882) | (121) | (1,882) | (1,902) |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 6,051 | 6,547 | 6,051 | 4,485 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 4,169 | 6,426 | 4,169 | 2,583 |


### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2022

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | ……………………. (Imesainiwa) | 22 April 2022 |
| Selemani Kijori **(Mkuu wa Fedha)** | ……………………. (Imesainiwa) | 22 April 2022 |
| Patrick Mashalla **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** ( | ……………………. Imesainiwa) | 22 April 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| "1/ Francis Ramadhani **(Mwenyekiti)"** | ……………………. (Imesainiwa) | 22 April 2022 |
| "2/ Enna V. Mwakipesile **(Mkurugenzi)"** | ……………………. Imesainiwa) | 22 April 2022 |




216826102

# Wazee 5,000 wapatiwa bima ya matibabu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga imetoa Bima za Afya ya CHF iliyoboreshwa kwa wazee 5,036 zenye thamani ya Sh. milioni 32.2 ili wapate matibabu bure.

Fedha hizo zimetolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2021/2022 na utoaji wa bima hizo unafanyika kila mwaka wa fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa kushirikiana na baraza la wazee wa manispaa hiyo.

Katibu wa baraza la wazee taifa, Anderson Lymo, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake kuhusu namna wanavyoshirikiana na halmashauri kuhakikisha kundi hilo linapata matibabu bure kwa kuwapatia bima za afya ya CHF iliyoboreshwa.

Alisema Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ina jumla ya wazee 6,692 na kati ya hao 5,036 wamepatiwa bima za afya ya CHF iliyoboreshwa na wazee 1,656 wanaendelea kupata bima hizo kupitia wadau wa maendeleo kwa kushirikiana na madhehebu ya dini yanayopatikana wilayani humo.

Lymo ambaye pia ni Katibu wa baraza la wazee la halmashauri hiyo alisema, mwaka wa fedha 2021/2022 unaoishia mwezi Juni mwaka huu, halmashauri hiyo iliwatengea Sh. milioni 4.5 kwa ajili ya kuwakatia bima hizo wazee 900.

Alisema kati ya bima hizo wazee wa kata ya Nyandekwa wapatao 100 watanufaika, Kagiongwa 60, Nyasubi 35, Busoka 34 huku kata za Kahama mjini, Isagehe, Mwendakulima, Mondo, Zongomela, Nyihogo, Nyahanga, Bukooba, Mhongolo, Majengo na kata ya Malunga watapata bima 40. "Sisi wazee tusiokuwa na bima ya afya tunapata shida pale tunapofika katika vituo vya afya au zahanati kupata matibabu na ndiyo sababu kubwa inachangia halmashauri kutenga fedha na kutupatia bima za CHF ili tukidhi mahitaji yetu kiafya," alisema Lymo.

Aliongeza kuwa kadi za CHF zinadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja na zinapoisha muda wake baadhi yao wanalazimisha kuzihuisha wenyewe na wale wasiokuwa na uwezo wanawaombea msaada kutoka kwa wadau ili kuzifufua waendelee kupata matibabu bure.

Mmoja wa wazee waliopata bima hizo, Abbas Hassan aliishukuru halmashauri kwa kuendelea kuwajali kila mwaka kwa kuwatengea fedha kwa ajili ya kuwakatia bima za afya na kwamba suala hilo linatakiwa kuigwa na halmashauri zingine hapa nchini.

Juma Salehe, alisema licha ya kupata bima hizo wanaomba pia kutengewa dirisha lao la wazee katika vituo vya afya na zahanati na kupewa daktari mwenye umri kama wao ili iwe rahisi kumueleza matatizo yao yanayowasibu wanapofika kupata matibabu.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala (kulia), akimtua ndoo ya maji Amina Suleiman, mkazi wa Pugu Mpakani, kama ishara ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye eneo hilo kupitia kukamilika kwa mradi wa Pugu Gongo la Mboto uliotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# RC ashukuru Kituo cha Afya Katoro kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule ameshukuru msaada uliotolewa kwa Kituo cha Afya Katoro.

Msaada huo umetolewa na Benki ya NMB ukiwa ni mwendelezo wa kusaidia sekta za elimu na afya nchini.

"Mmeendelea kuwa msaada mkubwa sana kwetu watu wa Katoro na Geita kwa ujumla, nashukuru sana benki yenu imekuwa ikitoa msaada sana kwa Serikali yetu," alisema Senyamule.

Alisema Benki ya NMB imekuwa kimbilio lao kila wanapokuwa wamepata changamoto, na kuahidi kuendelea kushirikiana nayo.

Kwa upande wake, benki hiyo iliahidi kuendelea kushirikiana na Serikali kuhakikisha wakazi wa Mkoa wa Geita wanazidi kupata huduma bora hasa katika sekta ya elimu na afya.

Ahadi hiyo ilitolewa na Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya msaada wa vitanda,magodoro na mashuka katika kituo cha afya Katoro pamoja na kutoa madawati 200, meza 50 na viti 50 kwa shule za msingi na sekondari katika mkoa wa Geita.

"Jumla ya msaada tuliotoa leo ni vitanda 10,magodoro 10, mashuka 30 kwa kituo cha afya Katoro, meza 50 na viti 50 kwa Shule ya Sekondari Magenge,Madawati 50 kwa Shule ya Msingi Msufini na Shule ya Msingi Bahari madawati 50, madawati 50 kwa Shule ya Msingi Mtakuja na madawati 50 kwa Shule ya Msingi Mchongamani na vifaa vyote vya vinathamani ya Shilingi milioni 30,". alisema Ladislaus.

Akimkabidhi vifaa hivyo Senyamule alimuhakikishia kuwa benki hiyo itaendelea kuchangia katika sekta hizi mbili kwani sera ya yake imeelekeza katika kuchangia maendeleo ya sekta hizo na kusaidia yanapotokea majanga.

# Chanjo ya polio kuwafikia watoto Songwe

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

Mkoa wa Songwe, umejipanga kuwafikia watoto wote wa umri ya chini ya miaka mitano (5) ili wapate chanjo ya matone na kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa polio ambao hivi karibuni umeripotiwa kuibuka nchini Malawi.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema hayo wakati wa kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi cha

Mkoa ambacho kimefanyika mwishoni mwa wiki kwa lengola kupeana uelewa juu ya kampeni ya chanjo ya polio kwa awamu ya pili mkoani humo.

"Lengo kuwafikia watoto wote wa umri chini ya miaka mitano, hivyo timu ya Afya itapita shuleni, nyumbani, sokoni, makambi na sehemu zote ambazo watoto watakuwepo"alisema Omary Mgumba.

Mgumba alisema chanjo ya polio inafahamika na Watanzania wengi vizuri, wazazi wanaijua na inatolewa kila siku kwa watoto kuanzia anayezaliwa hivyo Serikali haitarajii kusikia upotoshaji kuhusu chanjo hiyo.

"Serikali kwa sasa imeongeza tahadhari na kinga kwa watoto wake baada ya tishio la ugonjwa wa polio kwa majirani zetu wa nchini Malawi lengo kuu ni kujikinga na maambukizi hayo," Omary Mgumba.

Pia, kutokana na Wilaya ya Ileje kuwa na walemavu wapatao 300 idadi ambayo inakadiriwa kuwa kubwa, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amewaagiza watalamu wa Afya kufanya tathmini ya kina

kwa walemavu waliopo ili kujua historia yao na kuja na majawabu ili Serikali ijiridhishe kama ulemavu wao umeshabihiana na Polio.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, alisema mahudhurio ya kliniki ya awali kwa mjamzito yamekuwa ni shida, kina mama kujifungulia nyumbani nayo inaweza kuwa chanzo lakini tunashukuru Mkuu wa Mkoa kwa kutoa maelekezo kwa watalamu kufanya tathimini ya kina juu ya walemavu wa Ileje.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Dkt. Boniface Kasululu, alisema kampeni ya chanjo ya polio inafanyika kwa nchi zote jirani, baada ya ugonjwa wa polio kutangazwa nchini Malawi Mkoa wa Songwe ulifanya kampeni ya utoaji wa chanjo ya kwanza na sasa serikali imeamua ifanye tena kutokana na hatari ya ugonjwa huo.


Shekhe Hussein Batuza aliwaagiza viongozi wa dini kwa kushirikiana na wadau wengine washirikiane kuondoa dhana potofu kuhusu chanjo hiyo.

Kampeni ya chanjo ya polio kwa awamu ya pili mkoani humo itazinduliwa rasmi Aprili 28 hadi Mei1,2022 huku wananchi wakitakiwa kuwapeleka watoto wao kupata chanjo hizo ili kukwepa athari zaidi baada ya nchi jirani ya Malawi kuwa na visa vingi vya wagonjwa hao.



Ukurasa 12

**Kwa juhudi hizi vijana watapenda taifa na Muungano**



Ukurasa 13

NDOTO YA MZAZI ITATIMIA?
Siasa zake Jaramogi Odinga na mwanawe Raila kama mapacha



Ukurasa 14

**SHEKHE THABITI KOMBO**
**Nguzo ya Mapinduzi, Muungano Zanzibar**


# siasa

JUMATANO APRILI 27, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


KUMEKUCHA UCHAGUZI CCM

# Wadau wanena kisa figisu kutawala

**Na Sabato Kasika**

CCM inaendelea na uchaguzi wa ndani ikiwa kwenye ngazi ya matawi, ambao hata hivyo, umekumbwa na sintofahamu baada ya kuwapo kwa tuhuma kuwa katika baadhi ya maeneo, makada wamenyimwa fomu za kuwania uongozi.

Hali hiyo imesababisha Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, kuagiza fomu kutolewa upya ili kuhakikisha kila kada anayetaka kugombea asiwekewe figisu za aina yoyote.

Kwa mujibu wa Chongolo, chama kinataka wale wote wenye dhamira ya kuchukua fomu wachukue bila kuwekewa vizuizi, kwa kuwa CCM si ya mtu na si chama cha maslahi binafsi, bali ni cha wanachama wote.

Anaelekeza viongozi wa ngazi zote wanapaswa kutimiza majukumu yao kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho kwa kuacha ubinafsi, badala yake waache kila mwenye nia ashiriki na wanachama wachague wanayempenda.

Baada ya kujitokeza figisu hizo ndani ya chama hicho kikongwe, Nipashe imezungumza na wadau mbalimbali wa demokrasia ambao wamezungumzia hali hiyo na kutoa ushauri wa kuwezesha demokrasia kushamiri.



Makamu Mwenyekiti wa CCM (Bara) Abdulrahman Kinana (kushoto) na Katibu Mkuu Daniel Chongolo. Viongozi hao wameshtukia figisu kwenye uchaguzi. **PICHA: MTANDAO**

### KUNA UBINAFSI

Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anasema kitendo cha baadhi ya viongozi wa CCM kuwanyima fomu makada wanaotaka kuwania uongozi, ni ubinafsi.

"Viongozi hao hawajasoma ishara za nyakati kwamba CCM ya sasa inataka demokrasia itamalaki zaidi, bado wanaendelea kuleta ubinafsi uliokuwapo miaka mitano iliyopita kwa kuwanyima nafasi na fomu wenzao?" anahoji Mwakagenda.

Anasema iwapo hali hiyo haitadhibitiwa, kuna uwezekano katika uchaguzi wa ngazi ya juu kukwamishana kukawa kwingi zaidi, kwa madai kwamba ni kawaida kwa baadhi ya makada wa chama hicho kutafuta ushindi wa mezani au kupendelewa.

"Kama unakumbuka, wakati anachukua nafasi ya Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Abdulrahaman Kinana alitaja majukumu matatu atakayoanza nayo , la kwanza likiwa ni pamoja na kuimarisha demokrasia ndani ya chama hicho," anasema.

Anafafanua kuwa Kinana alijua demokrasia ndani ya chama hicho, ilipotea na kwamba kitendo cha baadhi ya viongozi kuwanyima fomu wagombea ni dalili tosha ya kuyumba kwa demokrasia ndani ya CCM." anadai.

Anaongeza: " Binafsi niliipenda hotuba ya Kinana, iliyojaa mausia mazito kwa wana CCM. Kwa mfano alihoji, kwani wanachama wakimchagua mtu sisi ni nani wa kupinga? Hivyo kama viongozi wangemuelewa wasingeleta ubinafsi kwenye uchaguzi unaoendelea kwenye chama hicho?" Anahoji.

### WOTE WAPEWE HAKI

Wakili Anna Henga, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), cha Dar es Salaam, akizungumzia hatua hiyo, anasema kila mwanachama ana haki ya kuwania uongozi ili mradi amekidhi vigezo vinavyohitajika.

Anasema, aidha, ana uhuru wa kutoa mawazo, kwa kuwa hakuna mwenye haki ya kumiliki mawazo ya mwingine, na kwamba hata katika suala la kuwania uongozi, ana haki ya kuchukua fomu kwa utaratibu uliowekwa na chama.

"Fursa za kuwania uongozi kupitia katika vyama iachwe huru kila mwanachama mwenye nia hiyo afanye kwa uhuru, kwa sababu ni haki yake, wasiwepo watu waozuia haki hiyo,"anasema Henga.

Wakili huyo anasema, CCM ni chama kikongwe ambacho makada wake wangeonyesha jinsi ambavyo demokrasia imeimarika ndani ya chama hicho kwa kuruhusu anayetaka kugombea aruhusiwe badala ya kuficha fomu.

"Ninaamini kwamba ili chama kiwe imara lazima demokrasia ndani ya chama iwe imara, lakini ninadhani wapo watu wachache ndani ya CCM wasiotaka demokrasia iwe imara, ndio maana wanaweka mizengwe," anasema.

### KUELEKEA PABAYA

Ikumbukwe kuwa Chongolo anatishia kuwa CCM haitasita kusitisha uchaguzi huo kwa ngazi zote za chama akiwaagiza makatibu wa wilaya kote nchini kuhakikisha katika uchaguzi huo vitumike vitabu vilivyohakikiwa kupiga kura na sio vinginevyo.

"Tunafuatilia, tukibaini kuna maeneo ambayo vitabu vilivyokuwa vimehakikiwa vimeongezwa majina ya watu wasiokuwemo kwenye utaratibu wa daftari la wanachama, wakurugenzi au makatibu wa uchaguzi watawajibika," anasema Chongolo.

**INAENDELEA UK. 12**

# Juhudi zinazowaelekeza vijana watapenda taifa na Muungano

**Na Gaudensia Mngumi**

DODOMA imezizima kwa maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, huku idadi ya raia na washiriki wengi wakiwa ni vijana waliozaliwa baada ya Muungano.

Kama ambavyo jitihada zinafanywa usiku na mchana kuwafanya wanafunzi wapende kujifunza hesabu, masomo ya sayansi na ya uchumi, kwa maelezo kuwa hayo ndiyo mambo muhimu katika dunia ya sasa.

Juhudi za kitaaluma zikiendelea inahitajika mikakati ya kuwafanya vijana wa Zanzibar na Tanzania Bara kupenda nchi zao na Muungano wao.

Kama ambavyo kila wakati serikali, wadau na wataalamu wanavyohimiza kusoma na kuitafuta sana elimu kadhalika juhudi zaidi zije kuwaelimisha watoto na vijana wa kupenda taifa na Muungano wao.

Ni kawaida vijana nchini kusikika wakisema Afrika Kusini au 'Souz' ni taifa bora na wengi kulitamani, mamia wameshatorokea huko.

Kadhalika wako wanaolia mchana na usiku kama ingewezekana wangekuwa wazamiaji na kuibukia Marekani au Ulaya wanapodhani ni sehemu bora ya kuishi kwa mafanikio makubwa.

Ian Kilenga mhandisi wa ujenzi na mchumi kutoka mkoani Kilimanjaro anapozungumza na gazeti hili namna bora kuwafanya vijana wawe wazalendo, anashauri wafundishwe mazuri ya nchi hii na upungufu ulioko kwenye mataifa wanayoyatamani.

"Hili ni jambo linalotakiwa kufanyika sasa. Vijana wanaamini kuwa Marekani kuna kila kitu na hakuna shida au umaskini kama ilivyo Tanzania. Ni fikra njema lakini kuna haja ya kuwafundisha ukweli kuhusu umaskini, njaa na dhiki kubwa wanayokuwa nayo wanaoishi kwenye mataifa wanayodhani ni 'supa'. "

Mathalani, anasema huko Ulaya wanapopatamani kuwa kuna utajiri mkubwa na watu ni mabilionea si mahali bora kama wanavyoamini.



Wakuu wa Muungano na umoja wa Tanganyika na Zanzibar, Aboud Jumbe na Mwalimu Julius Nyerere (kulia) wakiwa kwenye harakati za kisiasa. **PICHA: MAKTABA**

> "Ni fikra njema lakini kuna haja ya kuwafundisha ukweli kuhusu umaskini, njaa na dhiki kubwa wanayokuwa nayo wanaoishi kwenye mataifa wanayodhani ni 'supa'.

Kilenga anatamani watoto na vijana wa Tanzania shuleni wafundishwe kuwa Tanzania ina mambo bora kama suala la bima ya matibabu mfano mwanafamilia anayefanyakazi anawachangia na kuwatibu jamaa zake, wengine lakini Amerika suala la sera ya bima ya afya ni gumu na hata sasa kelele zimebakia kwenye bima ya afya ya Obama Care.

"Si hivyo tu kuna mambo mengi ambayo yapo Tanzania lakini huwezi kuyapata popote hata huko Afrika Kusini. Ni watu wachache Tanzania wasio na makazi, lakini huko ni mamilioni hawana pakulala- wakiitwa 'homeless'."

Anasema walimu shuleni na wadau waelezee uzuri wa taifa hili na kufafanua zaidi umuhimu wa Muungano na kwa ujumla kuhimiza watoto na vijana kupenda umoja na ushirikiano.

Kilenga anasema: "Ulaya leo inapenda kushikamana zaidi ndiyo maana kuna sarafu ya Yuro, visa ya Shengeni, usafiri wa treni wa tiketi moja unaoiunganisha Ulaya karibu yote. Wanazungumzia umoja siyo utengano licha ya Uingereza kujiondoa kwenye EU,"

Anakumbusha kupambana na fikra kuwa Muungano unakandamiza upande mmoja wa nchi washirika, akihimiza vijana kuonyeshwa mifano dhahiri ili kuangalia namna ulivyojenga umoja, udugu na watu kuendelea kupendana.

Anasema kila kitu kwenye Muungano kimewezekana na uwekezaji umewainua wafanyabiashara wengi kutoka Zanzibar na Bara ambao wamefanikiwa kimaisha kupitia Muungano.

**KILIO CHA AJIRA**

Vijana wengi wanakabiliwa na maisha magumu, hawana kazi, riziki na hawawezi kumudu maisha yao, wataupendaje Muungano na nchi zao kama maswali haya magumu hayatajibiwa?

Mchumi Seushi Lodger, kutoka Dar es Salaam, anashauri kuanzisha kampeni za kuhimiza vijana kufahamu kuwa hakutakuwa na maisha bora na ya raha kama wanazozitamani wakiamini kuwa zipo nchini Marekani, Afrika Kusini na Ulaya bila kufanyakazi kwa bidii.

Anaongeza: "Waambiwe iwe shuleni, nyumbani , kwenye mikutano ya kijamii na kisiasa kuwa hakuna aliyeondoa umaskini kwa kukaa kijiweni, kupiga hadithi vibarazani, chini ya miti kama wanavyofanya wengine wengi, akapata maendeleo."

Ludger anasema kuona kuwa kuwa nchi haina manufaa kwa vijana kwa sababu hakuna kazi, wala pesa miongoni mwao kwa kiasi kikubwa kunatokana na fikra za kutegemea wahisani au wafadhili bila vijana wenyewe kujituma na kujishughulisha.

"Tuwe na utaratibu wa kuwafundisha vijana wetu kujichunguza kila siku kuwa na rekodi kuanzia asubuhi hadi jioni kuandika walichofanya na kiasi cha fedha walichopata waache kukaa vijiweni kujadili Yanga na Simba au ligi za Ulaya. Hazi wasaidii. Waanze kuwajibika kwa ajili ya maisha yao." Anasema.

**UZALENDO ULIOPITILIZA**

Anasema Tanzania na Zanzibar ya leo inahitaja kutumia mikakati ya uzalendo uliopitiliza au 'jingoistic' kuzisemea zaidi kwa uzuri nchi hizi na Muungano kuliko mataifa mengine ikibidi kuzikanusha taarifa za kiupotoshaji zinazosifia mataifa mengine.

Wakilisifia taifa flani kuwa limejaa ajira, maisha bora kwa vijana ni vyema kukanusha taarifa hizo kwa kuonyesha uhalisia mfano vita dhidi ya wageni, kuharibu mali za wengine, ujambazi na mauaji yanayotokea kwenye mataifa wanayotamani kuyakimbilia.

## Kumekucha uchaguzi CCM; wadau wanena kisa figisu kutawala

**INATOKA UK. 11**

Pamoja na hayo, anawaagiza makatibu wa wilaya zote na maeneo yote ambayo wamebaini kuna figisu hizo, mchakato huo urudiwe ili kuhakikisha kila mwanachama mwenye nia ya kuwania uongozi asibaniwe.

Kwa mkoa wa Dar es Salaam anataja baadhi ya maeneo hayo kuwa ni Tandika wilayani Temeke, Manzese na Kimara wilayani Ubungo na kuagiza fomu zigawiwe upya kwa kuwa baadhi ya makatibu wa matawi kwa maslahi yao binafsi wamezuia baadhi ya wanachama kuchukua fomu.

"Dhamana tulizonazo hazijatupa haki ya kufanya uamuzi kwa ubinafsi, maeneo ambayo tumegundua yana hiyo changamoto napiga marufuku kuwanyima fomu wanachama," anasema.

**FIGISU NI MAZOEA?**

Mtindo wa wanasiasa kufanyiana figisu unaelekea kuota mizizi kwani si mara ya kwanza kuzisikia, bali zimewahi kutokea hasa unapofanyika uchaguzi unaoshirikisha chama tawala na upinzani.

Uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 ni mfano mojawapo ambapo baadhi ya wagombea walifanyiwa 'figisu' ikiwamo kunyimwa fomu au fomu zao kutopokelewa kwa madai kwamba wamerejesha nje ya muda.

Kutokana na hali hiyo, vyama vya upinzani vikiwamo vya CHADEMA, UMD, CCK, NCCR-Mageuzi, NLD, ACT-Wazalendo, CUF na CHAUMA, vilitangaza kujitoa kushiriki kinyang'nyiro hicho.

Uamuzi huo ulitokana na malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa mbele ya umma na kulaumu CCM kuwa chanzo cha kusababisha hayo yote katika uchaguzi huo wa mwaka 2019.

Aliyekuwa mwenye dhamana ya uchaguzi wakati huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Seleman Jaffo, ambaye kwa sasa yuko Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, alijitahidi kuviomba vyama vya upinzani kulegeza msimamo na kutaka wagombea walioteuliwa waendelee na uchaguzi huo, jitihada hizo hazikuzaa matunda kwa vile havikukubali wala havikushiriki.

NDOTO YA MZAZI ITATIMIA?

# Siasa zake Jaramogi Odinga na mwanawe Raila kama mapacha

**Na Chiristina Mwakangale**

MZEE Jaramogi Ajuma Oginga Odinga alizaliwa mwaka 1911, alikuwa mwalimu, mfanyabiashara, mwanasiasa na kiongozi wa Waluo nchini Kenya, pia Makamu wa Rais wa Kwanza wa nchi hiyo.

Anatokea Bondo jimbo la Nyanza na baada ya elimu yake sekondari aliendelea kusomea ualimu katika Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda tangu mwaka 1939, baadaye akawa mwalimu mkuu.

Odinga alijitahidi kujenga umoja kati ya Waluo wa Kenya pia huko Uganda na Tanzania. Anaheshimiwa kwa kuitwa "Ker" au kiongozi wa kiroho. Wakati ule alipewa jina la "Jaramogi" au "mwana wa Ramogi" aliyekuwa Ker katika karne ya 16 akikumbukwa sana kwa Waluo.





Mzee Jaramogi Ajuma Oginga (kulia) Odinga na mwanaye Raila Odinga.. **PICHA: MTANDAO**

### BABA ALIPOANZA SIASA

Mwaka 1947 akaanzisha kampuni yake Luo Thrift and Trading Corporation na mwaka huo huo akaingia katika siasa akiwa Mjumbe wa Baraza la Ushauri wa Koloni. Akajiunga na chama cha Kenya African Union (KAU).

Wakati wa vita ya Maumau, Waingereza waliwakamata kiongozi Jomo Kenyatta na Odinga alibaki mtetezi wa harakati hizo za uhuru.

Mwaka wa 1960 walikuwa waanzilishi wa chama cha KANU akampendekeza Kenyatta kuwa kiongozi mkuu na baada ya uhuru, Odinga alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na 1964, Makamu wa Rais Kenyatta. Kiitikadi alionekana Mjamaa, akipinga siasa za viongozi wengine wa KANU waliolekea mrengo wa kulia.

Wakaanza kutofautiana hata na Mkuu wake, Mzee Kenyatta. Mwaka 1966 mkutano wa KANU ukafuta nafasi ya Makamu wa Mwenyekiti wa chama na Aprili 1966, Mzee Odinga akajiuzulu katika serikali na kuanzisha chama chake cha Kenya People's Union (KPU).

Ukaingia msuguano wa chama kipya dhidi ya serikali na mwaka 1969 kulitokea ugomvi Kisumu wakati wa ziara ya Rais Kenyatta na Odinga aliwekwa jela kwa miezi 15. Baadaye alibaki yu mpinzani na baada ya kifo cha Mzee Kenyatta, Rais mpya Daniel Arap Moi, alimrudisha Odinga katika KANU na kumpa cheo kama Mwenyekiti wa Bodi ya Kilimo.

Hata hivyo, hapakuwa shwari na Odinga alijaribu kuunda chama kipya na wakati ule Kenya ikatangazwa kuwa nchi ya chama kimoja tu.

### MAGEUZI 1990

Kuporomoka mfumo wa chama kimoja 1990/1991, Mzee Odinga alianzisha chama kipya NDP, akatupwa tena jela. Alipotoka akaanzisha chama cha FORD kilichounganisha wapinzani wengi wa Moi.

Mzee Odinga alipotoka, akawa kiongozi wa kitengo kimoja na aliposhiriki uchaguzi wa rais mwaka 1992, alishika nafasi ya nne.

Mfarakano wa upinzani ulimwezesha Moi kurudi kwa asilimia 35 ya kura zote. Kuundwa FORD kulikuwa mwanzo wa mabadiliko ya mageuzi ya kisiasa kutokea katika uchaguzi mwaka 2002.

Mzee Odinga hakuyaona mafanikio hayo, akafariki Januari 1994, akiacha wanawe wawili wanasiasa; Raila na Oburu Odinga, aliyeshika ubunge nchini humo na katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### SAFARI YA MTOTO

Raila alizaliwa mwaka 1945 nchini Kenya. Ana mke na watoto wanne. Alipomaliza shule Kenya, alienda kusomea uhandisi mitambo katika Chuo cha Ufundi Magdeburg Ujerumani, kati ya mwaka 1965 hadi 1970.

Baada ya hapo, akawa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi hadi mwaka 1974, alipohama ajira, kuwa Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Kenya.

Mwaka 2008, Raila alianzisha kampuni zake, pia akiendesha kampuni za familia, zikiwamo ya mjini Kisumu inayotengeneza chupa za gesi ya kupikia. Mwaka 2007, alikadiriwa kuwa na mali zenye thamani Sh. bilioni nne za Kenya. Binafsi ni shabiki mkubwa wa soka na mara nyingi hushiriki mechi za timu ya Bunge la Kenya na mikutano ya kisiasa huwaiga watangazaji soka redioni.

### MAISHA YA SIASA

Raila alionekana katika siasa mara ya kwanza baada ya jaribio la mapinduzi ya kijeshi mwaka 1982 nchini Kenya. Alishtakiwa kushiriki mipango, hata akawekwa kifungo cha nyumbani miezi sita na kisha akakaa jela jumla ya miaka minane, vipindi tofauti:1982-1988; 1988-1989 na 1990-1991..

Mwaka 1991, Raila alikimbilia nchini Norway, akihofia maisha yake. Baada ya serikali kubadilisha katiba na kuruhusu vyama vya upinzani, akarudi na kujiunga na chama cha Ford kilichoongozwa na baba yake. Katika uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi, alichaguliwa mbunge wa Lang'ata, jijini Nairobi.

Mafarakano yalipotokea ndani ya Ford, alibaki kambi ya baba, Ford-Kenya, nyingine ikiitwa Ford Asili. Baada ya kifo cha baba yake, akagombea uongozi wa Ford-Kenya akashindwa na Michael Wamalwa. Hapo akahamia chama kidogo cha National Development Party (NDP) akifuatwa na wabunge wengi wa kabla lake, Waluo.

Katika uchaguzi 1997, alishika nafasi ya tatu, akitanguliwa na Moi na Mwai Kibaki. Akawa mbunge wa upinzani, huku akijenga maelewano na Rais Moi na chama chake KANU.

Wapinzani wa Raila, walimponda analinda maslahi ya biashara zake, huku waliomtetea walidai upinzani uligawanyika mno, akaona aungane na watawala.

Mwaka 2001, Raila aliteuliwa Waziri wa Nishati, naye akaendelea kuunganisha chama chake NDP na KANU, hata akawa Katibu Mkuu wa muungano huo.

Kabla ya uchaguzi 2002 mfarakano ukaibuka, Raila akitegemea kuteuliwa kugombea urais wa KANU mpya, lakini Rais Moi akatangaza chaguo lake ni Uhuru Kenyatta.

Raila, pamoja na sehemu ya viongozi wa KANU waliondoka kujiunga na upinzani uliowahi kuunga mkono chini ya bendera ya National Alliance of Kenya (NAK).

Akiwa na viongozi wa KANU; Kalonzo Musyoka, George Saitoti, Joseph Kamotho wakatangaza kuundwa kwa harakati uitwao Rainbow Movement (upinde wa mvua). Walitumia chama kidogo Liberal Democratic Party (LDP) kama chombo cha kisheria kwa umoja wao mpya na waliingia majadiliano na NAK iliyokuwa muungano wa vyama vya upinzani, wakaunda umoja mpya NARC (National Rainbow Coalition).

"Katika mkutano mkuu wa ODM Raila alipata kura nyingi kuwa mgombea wa urais. Musalia Mudavadi, William Ruto na Joseph Nyagah wakaamua kushikamana naye wakabaki katika ODM.

NARC ikamsimamisha Marehemu Mwai Kibaki, wakimpigia debe "Kibaki tosha" akifafanua yeye kutoka kabla la waluo, anamuunga mkono na mgombea Mkikuyu, yaani Kibaki.

Msingi wa ushirikiano huo ulikuwa mapatano yaliyoitwa "Memorandum of Understanding" ikiwa na maudhui:Kibaki atakuwa rais LDP itapewa nusu ya mawaziri katika serikali; ndani ya siku 100 katiba itabadilishwa itakayopunguza madaraka ya Rais; sehemu ya madaraka ya rais zitakabishiwa kwa cheo kipya cha waziri mkuu; Raila atakuwa Waziri Mkuu wa NARC.

NARC ikashinda uchaguzi na Kibaki akawa rais mpya, Raila akiwa Waziri wa Barabara. Lakini, Kibaki hakutimiza, kwa LDP kupatiwa nusu ya mawaziri.

Mkutano wa kusahihisha katiba ulikwamishwa na mapendekezo ya mkutano wa kutunga katiba mpya hayakutekelezwa, cheo Waziri Mkuu hakikuanzishwa.

Mwaka 2005 upande wa Rais Kibaki ulijaribu kuanzisha katiba mpya usiokuwa na mabadiliko mengi kwenye madaraka ya rais. Cheo kipya cha Waziri mkuu kikapangwa ila kikiwa na madaraka kidogo; na ugatuzi wa madaraka.

Kampeni ya kura ikagawa taifa, mawaziri wa serikali walionekana pande zote mbili. Watetezi wa katiba iliyopendekezwa walitumia ishara Ndizi na wapinzani ishara Chungwa. Raila akiwa na KANU kilichokuwa chama cha upinzani tangu 2002, wakafaulu kuzuia katiba kwa kura ya wananchi wote.

Kibaki akajibu kwa kuachisha mawaziri wote. Raila na Uhuru wa KANU waliunda harakati mpya ya ODM (Orange Democratic Movement) ili kugombea urais.

ODM nayo ikapata mafarakano ilipotaka kumteua mgombea wa urais. Kalonzo Musyoka na wafuasi wake kutoka Ukambani walijiondoa Agosti 2007 wakaanzisha ODM-Kenya.

Katika mkutano mkuu wa ODM Raila alipata kura nyingi kuwa mgombea wa urais. Musalia Mudavadi, William Ruto na Joseph Nyagah wakaamua kushikamana naye wakabaki katika ODM.

Mabaki ya KANU chini ya Uhuru Kenyatta, wakajiondoa katika upinzani wakahamia upande wa Rais Kibaki. Katika kura za maoni Septemba 2007, Raila alionekana mbele. Odinga alitangazwa na ODM kama mshindi na mfarakano mkubwa ulitokea, hasa maeneo ya Bonde la Ufa.

Baada ya vifo vya watu na uchumi kudhurika nchini Kenya, hali hiyo iliingiliwa kimataifa, pande zote mbili chini ya mpatanishi Kofi Annan yalifikia maelewano ya kuundwa serikali ya umoja, Kibaki akiwa Rais na Raila Waziri Mkuu. Raila Odinga, mwaka 2022 sasa kaibuka tena kuwania urais mara ya tano kwa tiketi ya Azimio la Umoja.

## SHEKHE THABITI KOMBO JECHA

# Nguzo ya Mapinduzi, Muungano

**Na Chiristina Mwakangale**

- Mshiriki, aliyefanikisha kung'olewa Sultan

JINA THABIT Kombo Jecha ni kubwa miongoni mwa waasisi wa historia, mapinduzi, utaifa na maendeleo ya demokrasia na uchumi Tanzania Bara na Zanzibar.

Shujaa huyu ana kila sababu ya kukumbukwa wakati huu wa maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliokuja baada ya Mapinduzi ya 1964 ambayo Kombo alishiriki na kuyafanikisha.

Ni mwanamapinduzi na mtetezi wa haki za Wazanzibari, aliyejitolea kupigania haki hadi kufikia ushindi, unaosherehekewa leo.

Shekhe Kombo aliyefariki mwaka 1986 kwa maradhi ya moyo, akiwa na miaka 82, ameacha pengo kwa Watanzania ambalo hawana cha kufanya mbali na kumuombea rehemu na msamaha kwa Mola. Shekhe Kombo alikuwa maarufu kwa neno 'weka akiba ya maneno' alilitumia kila aliposisitiza jambo la msingi alitunukiwa kipawa kikubwa cha busara, hekima na upambanuzi wa hali ya juu wa mambo.

Siku zote yeye alikuwa ni mtu wa kati na akitumika kusuluhisha penye matatizo na kuleta mshikamano pale penye utengano.

Januari 12, kila mwaka, Zanzibar inaadhimisha Mapinduzi yaliyouondoa utawala wa kisultani visiwani humo yakiwahusisha wakwezi na wakulima walioungana kwa sauti moja na kusema: uonevu sasa basi.

"Tunataka visiwa vyetu vilivyotawaliwa kwa miaka mingi bila ridhaa yetu virejee mikononi mwetu ."

Katika kitabu kiitwacho 'Masimulizi ya Shekhe Thabit Kombo Jecha,' maneno au kauli za mwanamapinduzi huyo zilizokusanywa na mwandishi, Luteni Minael-Hosanna Mdundo, kinaelezea kwa kina namna alivyokuwa na mchango katika historia ya visiwa hivyo maarufu kwa utalii.

Kitabu kimesheheni nyaraka mbalimbali muhimu za kihistoria, utangulizi wake uliandikwa kwa ustadi mkubwa na Baba wa Taifa na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere.

Mara nyingi Nyerere na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Shekhe Abeid Karume walipokwama katika masuala mbalimbali, mshauri wao mkubwa alikuwa Thabit Kombo na hata Mwalimu baada ya kustaafu, alimtumia kwa mambo mengi ya kisiasa na ushauri mwingine.

Kwa maneno yake mwenyewe Mwalimu kwenye utangulizi wa kitabu hicho, anasema:

"Shekhe Thabit Kombo ndiye aliyependekeza Karume awe kiongozi wa chama kipya Afro Shirazi Party (ASP). Karume, naamini kwa moyo na nia safi kabisa, hakutaka kuwa kiongozi wa chama kipya hicho."

"Bila busara, hekima na ujasiri wa Shekhe Thabit, pengine vyama hivyo ASP na Shirazi Association visingeungana au kama vingeungana, baadaye ungetokea mzozo kuhusu uongozi."

"Shekhe Thabit, alikuwa kiongozi mpendwa, mwenye sifa njema, aliyependwa na watu wa kila rika kwa ushauri... alikuwa radhi wakati wote kuwasikiliza wanyonge na wakati mwingine hata kuwavumilia wajinga na wakorofi kwa kiwango cha kushangaza.



Thabit Kombo Jecha, Katibu Mkuu wa ASP enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

> Saa 5:00 asubuhi Januari 11, 1964, ulikuwa ndiyo wakati wa kukamilisha mipango yote na kufanya marekebisho ya mwisho kama hapana budi.

"Nyumbani kwake na ofisini palikuwa mahali pa watu wa kila aina kuchota busara, wakiingia na kutoka mchana na usiku."

### KOMBO NI NANI?

Shekhe Thabit Kombo, alizaliwa Kizimkazi mkoa wa Kusini Unguja mwaka 1904, hakubahatika kusoma sana elimu ya darasani Nyerere anasema aliishia chumba cha nne , lakini Mwenyezi Mungu alimjalia kipaji kikubwa cha kujifunza na kuzungumza kwa ufasaha hata kuweza kuwashawishi watu wenye mioyo migumu kuungana na vyama vya ukombozi wa Zanzibar na vya Afrika.

Sababu kubwa ya kufanyika mapinduzi ya mwaka 1964 ni madhila ya Waarabu waliyowafanyia wakazi wa Zanzibar, ambayo mengine hayasimuliki kwa namna yalivyokuwa mabaya.

Katika mazungumzo yake na Luteni Minael-Hosanna kuhusu Mapinduzi ya Januari 1964, Shekhe Kombo anasema: Usiniulize vijana wetu walioendesha Mapinduzi walipata wapi mafunzo au nani hasa alivamia mahala gani. Mimi sijui.

"Nasikia hadithi tu kila mmoja akijinasibu baada ya kushinda, mengine ya kweli na mengine ya uwongo mi-sijui ninachojua mimi ni kwamba Kamati Kuu ya ASP (wakati huo yeye akiwa ni Katibu Mkuu wa ASP ilisononeka baada ya mkutano wa pili wa London uliojadili uhuru wa Zanzibar na kuendelea kumpa Sultani mamlaka).

"Tumesononeka kwa sababu matumaini yetu yote ya kuupata uhuru wa nchi yetu kwa njia ya kura yalikuwa yamefutika; Hatimaye tukazaa shauri kwamba baada ya uhuru huo bandia wa Desemba 10, 1963, Kiongozi Mkazi Mwingereza akitoka tu, basi tushike mapanga tumng'oe Sultani.

Anasema uamuzi huo wote ulikuwa na kauli moja katika siri kubwa na Mwenyezi Mungu akawabarikia katika dua hiyo.

Hata hivyo, Mapinduzi hayakuwa rahisi bali kuliingia fitina nyingi ambazo kwa namna moja au nyingine zilianza kuwakatisha tamaa Wanamapinduzi hao.

Shekhe Kombo, anaelezea kisa kimoja usiku wa kuamkia siku ya Mapinduzi.

"Saa 5:00 asubuhi Januari 11, 1964, ulikuwa ndiyo wakati wa kukamilisha mipango yote na kufanya marekebisho ya mwisho kama hapana budi. Tukakutana Shekhe Karume, Aboud Jumbe na mimi, viroho vinatudunda.

"Mimi nilikuwa nimepata fununu kuwa huenda mipango yetu imegundulika. Basi baada ya mkutano wetu, nikamshauri Shekhe Karume kwa hii habari yetu ya Mapinduzi inaonekana imeenea katika mji mzima, watu wanaizungumza, Aboud Jumbe naye akathibitisha kuwa na yeye kaisikia Miembeni. Basi tukaulizana tufanyeje," anaeleza Shekhe Kombo.

Katika maelezo yake anasema walikubaliana kumuita Ofisa wa Polisi Unguja, wamweleze kuwa kuna watu wanataka kufanya vurugu mjini, hivyo polisi waimarishe ulinzi, kufanya hivyo ni kuwa ili machafuko yakitokea basi wao wawe katika mikono salama.

"Kumbe fikira ile ya kumwita Superintendent (Ofisa wa Polisi) ilikuwa mbinu ya kufaa sana, maana askari waliokuwako Bomani walipunguzwa nguvu na vikosi vya Mapinduzi vikaweza kuingia Bomani kwa urahisi na kuchukua silaha."

Kwa maelezo ya Shekhe Kombo, vikosi vya Mapinduzi viliingia maeneo ya mjini ambako siku hiyo kulikuwa na sherehe ya 'Fete' kuanzia saa 10 jioni, sherehe ilifanyika na watu wa kila rangi walikusanyika kwa furaha bila hofu. Sherehe hiyo iliandaliwa na ASP ili kuwawezesha wakulima na wakwezi waliokuwa wakiishi mashambani, kuingia Unguja mjini bila vikwazo au vizuizi kutoka serikalini kama ilivyokuwa kawaida hasa nyakati za jioni kipindi hicho.

Kama walivyoagizwa na utawala wa Kisultani kuwa sherehe ilipaswa kuisha saa 6:00 usiku, ulipotimu muda huo, ngoma zikazimwa na hapo ndipo ikawa mwanzo wa utekelezaji wa mipango ya Mapinduzi.

"Kwa mawe, marungu na mapanga, vijana hawa wakawa na ujasiri wa kushambulia makao makuu ya Jeshi la Polisi na kuyateka haraka haraka. Halafu wakakamata Ziwani. Hapo walipata silaha nyingi na walikuwapo waliokuwa wanajua kuzitumia, hivyo hivyo wakateka kituo cha Mtoni.

"Kivumbi kikawa Malindi, kule kulitokea mapambano makali, lakini moyo wa vijana wa ASP ambao sasa walikuwa wanatumia silaha za moto au bunduki walizokuwa wamejinyakulia Ziwani na Mtoni, ukawasukuma hadi wakashinda. Haukupita muda wakawa wameikamata Malindi pia.

"Rahaleo ndiko kulikokuwa Makao Makuu ya Mapinduzi na Shekhe Karume alikuwa kule kutokea usiku hadi alfajiri wakati sehemu zote muhimu zimekwisha kushikwa na vijana wetu wote wanazo silaha. Sasa Mapinduzi yakatangazwa katika Sauti ya Zanzibar," anasimulia Shekhe Kombo.

Awali Shekhe Kombo, alimtaja John Okello, Abdallah Natepe na Yusuf Himid kama miongoni mwa vijana waliokuwa mstari wa mbele katika kutekeleza Mapinduzi, lakini akikiri kutomfahamu vyema Okello.

### SULTANI KUTOROKA

Kuhusu Sultani kuikimbia Zanzibar wakati wa Mapinduzi, Shekhe Kombo anasimulia: Sultani hakukamatwa. Wakati vijana wanashughulikia vile vituo muhimu, yeye akapata nafasi ya kupuruchuka na kukimbilia melini na meli yake ikaeleaelea karibu na Unguja kwa muda mrefu.

"Kwa bahati Mwalimu Nyerere akaombwa na serikali ya Uingereza amhifadhi Sultani hadi hapo mipango ya kumsafirisha itakapokamilika."

"Na Mwenyezi Mungu akampa Mwalimu Nyerere busara kubwa ya kulikubali ombi hilo haraka. Kutahamaki, Sultani ameshafika Dar es Salaam, mgeni wa Mwalimu Nyerere."

"Hata sisi viongozi wa ASP tulikuwa na hofu juu ya Sultani aliyepuruchuka, kama angepata akili kwenda Pemba na halafu kutoka kule akaomba msaada wa majeshi kutoka nchi za nje, hali yetu ingekuwa ngumu sana."

**TAARIFA MBALIMBALI**





## Kabaka atoa angalizo upangaji safu CCM

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi (UWT), Gaudensia Kabaka, amewaonya watendaji wa umoja huo kutopanga wagombea na washindi wa chaguzi zinazoendelea ndani ya CCM na jumuiya zake.

Aidha, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutangaza utalii na kutoa wito kwa watanzania kufanya utalii wa ndani ili kuchangia pato la taifa. Kabaka alisema watendaji hao wanapaswa kutokuwa sehemu ya kupanga wagombea na washindi kwa kuwa hali hiyo husababisha makundi ndani ya chama.

"Kwa sasa kuna chaguzi mbalimbali zinaendelea ndani ya chama na jumuiya zake nitoe wito kwa wanawake, wanaume na vijana kujitokeza kushiriki ipasavyo kwenye uchaguzi na kuchagua viongozi mnaowataka, lakini kwa watendaji wetu wasiwe sehemu ya kupanga wagombea ili kujiepusha kusababisha makundi,"alisema.

Kuhusu ziara ya Rais Samia Marekani, alipongeza kwa kuleta matokeo chanya nchini ambapo ameshuhudia utiaji saini wa uwekezaji wa zaidi ya Sh.Trilioni 11 utakaofanyika Tanzania.

"Kama mnavyojua Rais wetu anafanya kazi kubwa sana ya kutangaza Tanzania kimataifa ambapo sasa ndege zitatoka moja kwa moja Dallas Marekani kuja Tanzania hii ni hatua kubwa sana, pia kuna uwekezaji wa matrilioni utafanyika hapa nchini, kuna kila sababu ya kumpongeza na kumuunga mkono Rais kwa jitihada anazofanya,"alisema.

Aliongeza kuwa "Rais amejitolea kwa hali ya juu kutambulisha Tanzania duniani, filamu ya 'Royal Tour' imeonyeshwa kwenye vituo vya televisheni 350 vya Marekani hii ni kazi kubwa na italeta matokeo chanya."

Alisema kazi hiyo ameifanya kwa uzalendo na unyenyekevu kwa maslahi ya taifa.

Akizungumzia kifo cha Mbunge wa Viti maalum, Irene Ndyamkama, alisema alikuwa Mbunge mwenye maono ambapo alikuwa akijenga nyumba ya Katibu wa UWT Mkoa wa Rukwa na kuahidi kuikamilisha na kuiwekea samani za ndani baada ya kujifungua.

# Gavana akosoa wanawake katika uhifadhi wa akiba

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, amesema pamoja na wanawake kuwa na uwezo mkubwa wa kujiwekea akiba kuliko wanaume, bado wanahifadhi sehemu zisizo rasmi zinazohatarisha usalama wa akiba zao.

Prof. Luoga alitoa kauli hiyo wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa kamati ya wanawake ya huduma jumuishi za fedha (WACFI).

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanawake ndiyo wamekuwa na uwezo wa kuweka akiba zaidi ukilinganisha na wanaume, lakini maeneo wanayohifadhi siyo rasmi.

"Wanawake ndiyo wenye uwezo mkubwa wa kuweka akiba kuliko wanaume, lakini sehemu wanazoweka akiba hizo mara nyingi ni majumbani eneo ambalo siyo rasmi lakini pia wakitaka kukopa wanatafuta rafiki ili amkopeshe na siyo katika taasisi rasmi za kifedha," alisema Gavana Prof. Luoga.

Aidha, alisema vikundi vingi vya kuweka akiba na kukopa nchini ni vya akinamama lakini namna vinavyoendeshwa vinaweza visiwe na tija kwao.

"Ni vizuri kama vinaweza kuandaliwa vizuri tukatafuta namna ya kuviweka ili akinamama siyo tuu kupata huduma bali huduma za fedha jumuishi zikaimarishwa ili kuwafikia wananchi wote,"alisema.

Vile vile, alisema akinamama pia wamekuwa waaminifu kwa taasisi za kifedha pale wanapokopa na kurejesha mikopo yao kwa uaminifu zaidi ya wanaume.

Akizungumzia umuhimu wa kamati hiyo, alisema ni kiungo muhimu cha shughuli mbalimbali zinazowalenga wanawake katika sekta za fedha.

"Huduma shirikishi za kifedha nchi yetu ni kinara katika bara la Afrika hata nchi za nje ya Afrika takwimu za mara ya mwisho zinaonyesha hata Sweden ilikuwa nyuma yetu sema tu tumelegalega hivi karibuni, lakini malengo yetu ni kuboresha huduma hizi ili kufikia kila mwananchi,"alisema.

Kadhalika, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya kufikisha huduma jumuishi za fedha kila eneo na kuwafikia watu wote wakiwamo wanawake.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, aliiagiza kamati hiyo kwenda kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi ili kuwasaidia wanawake katika huduma jumuishi za fedha.

"Wanakamati nimeambiwa mpo 11, mliochaguliwa lazima mhakikishe kuwa mnakwenda kufanya kazi ili waliowachagua kuendelea kuwaamini mkasaidie wanawake kufikiwa na huduma jumuishi za fedha ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi hasa waliopo vijijini,"alisema.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Beng'i Issa, alisema kamati hiyo ipo tayari kwenda kutekeleza majukumu yake ya kuimarisha huduma jumuishi za fedha kwa wanawake nchini.




Mtaalamu wa kudhibiti majanga kutoka mgodi wa Barrick North Mara, Samwel Nyansika, akitoa elimu jinsi ya kuzima moto kwa askari wa kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), Mkoa wa Dodoma jana. Kampuni hiyo, pia ilitoa msaada wa vifaa vya kuzima moto kwa kikosi hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati kupambana na malaria waja na kibano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu ametangaza mkakati kitaifa wa kupambana na malaria nchini ambapo kaya itakayobainika kuwa na dimbwi au vichaka vya majani ndani ya mita tano, hatua zitachukuliwa ikiwamo kuwatoza faini.

Aidha, amesema kipimo cha malaria na dawa aina ya ALU ni bure na kutoa wito kwa wananchi kupima badala ya kunywa dawa kiholela.

Waziri Ummy aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani ambayo kitaifa ilifanyika jijini hapa.

Alisema anaandaa waraka na kuuwasilisha Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kuupeleka kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza mkakati huo.

"Hatuhitaji mdau kutuambia safisha nyumba yako, wa kusema tuondoe madimbwi yanayozunguka nyumba yako nimeambiwa hapa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Dk.Binilith Mahenge alikuja na sera ya mita tano kulia, kushoto, nyuma, mbele ndani ya mita tano lazima nyumba yako iwe safi nabariki mkakati huu, kuwa wa kitaifa wa kupambana magonjwa ya mbu,viroboto,"alisema.

Alisema kila nyumba ihakikishe mazingira yanakuwa safi zisizungukwe na madimbwi au vichaka vya majani vinavyozalisha mbu wa malaria.

Aidha, aliagiza Maofisa Afya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyoo bora na kuondoa madimbwi yaliyopo umbali wa mita tano kutoka kwenye makazi ili kuua mazalia ya mbu na kutokomeza malaria.

Pia alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wadau pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI, inatekeleza Mpango Mkakati wa Malaria wa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2025, unaolenga kupunguza kiwango cha maambukizi ya Malaria nchini kutoka wastani wa asilimia 7.5 ya mwaka 2017 hadi kufikia wastani wa chini ya asilimia 3.5 ifikapo mwaka 2025.

"Mpango huu una mikakati mikuu mitatu ni pamoja na udhibiti wa mbu waenezao malaria, uchunguzi, tiba na tibakinga ya malaria kwa makundi maalum, na ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa ugonjwa wa Malaria hapa nchini," alisema.

Akizungumzia upuliziaji wa dawa kwenye kuta, Waziri huyo alisema kwa sasa utafanyika kwa Halmashauri 61 ambazo zipo kwenye Mikoa sita yenye mzigo mkubwa wa maambukizi ya malaria.

"Mikoa inayoongoza kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya Malaria ni Mkoa wa Kigoma wenye asilimia 24; Mkoa wa Geita wenye asilimia 17; Mikoa ya Kagera na Mtwara yenye asilimia 15; Mikoa ya Lindi na Ruvuma yenye asilimia 12,"alisema.

Hata hivyo, alisema Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Njombe na Iringa ina kiwango cha chini cha maambukizi ya Malaria chini ya asilimia moja.

"Hatuwezi kumaliza malaria kwa kugawana vyandarua nyie wenyewe ni mashahidi, wale mbu wanaosambaza malaria wa usiku wa manane wamebadilika, siku hizi mbu anaweza kukuuma kabla ya kupanda kitandani, ndiyo maana hivi vyandarua tunavyotoa vyenye dawa siku hizi vinashindwa kuhimili baadhi ya mbu,"alisema.

Kadhalika, alisema kuna kifaa kipo hatua za mwisho kukaguliwa ambacho kikihifadhiwa ndani ya chumba kitafanya kazi ndani ya miezi tisa.

"Vipimo na dawa za malaria, vinatolewa bila malipo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma. Watoa huduma wahakikishe huduma hizi zinaendelea kutolewa bila malipo...Ndani ya wiki mbili tutatoa mwongozo."

Kuhusu takwimu za malaria, Ummy alisema "Najisikia vibaya kusema vifo vitokanavyo na malaria tumepunguza kwa asilimia 71, kwangu mimi naona aibu kusema hizi takwimu kwa sababu wananchi ambao wanapata huduma za kupima malaria ni asilimia 43 tu, tuna lundo la wananchi hawajapima,"alisema.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Dk.Grace Magembe, alitaka viongozi wa Mamlaka za serikali za mitaa kutumia ipasavyo fedha zinazopelekwa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za kupambana na malaria.



# Homera ataka Muungano kuendelea kuenziwa kote

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka wananchi wa Mkoa huo kuendelea kuuenzi na kuulinda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulizaa taifa la Tanzania, kwa kuhakikisha miradi yote ya maendeleo iliyoanzishwa inaendelea kunufaisha vizazi na vizazi.

Homera ametaja miongoni mwa miradi hiyo ni Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Homera alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na waandishi wa habari, katika kuadhimisha miaka 58 tangu kuanzishwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuzaa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema miongoni mwa mambo yanayopaswa kuenziwa ni pamoja na uanzishwaji wa Reli ya Tazara ambayo hadi sasa licha ya kukuza uchumi wa Taifa, pia umechangia kuimarisha mahusiano mazuri kati ya Zambia na Tanzania na mataifa mengine ambayo hutumia reli hiyo kusafirisha biashara zao.

"Bado tunaendelea kumuenzi baba wa Taifa letu la Tanzania, ni mengi kayafanya hadi sasa tunayaishi ikiwamo kuboresha miundombinu ya barabara na reli, aliweka msingi mzuri ndiyo maana hata viongozi wetu wa kitaifa sasa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maono ya Hayati Mwalimu Nyerere, nawaomba wanaMbeya tuendelee kumuombea Mungu aendelee kumpa pumziko la amani," alisema Homera.

Aidha Homera alisisitiza wanambeya na Taifa kwa ujumla kuendelea kuenzi Muungano huo ambao umelifanya Taifa la Tanzania kuendelea kuwa kisiwa cha amani na kukua kila siku kiuchumi, kwa sababu wananchi wanafanya shughuli zao katika mazingira ya utulivu.

Alisema asiwapo Mtanzania yeyote atakayejaribu kupenyeza maneno yenye chuki yanayochochea kuharibu Muungano kwa maelezo kuwa jambo hilo lina gharama kubwa kwa ustawi wa maisha ya Watanzania.

Alisema katika kumuenzi Hayati, Mwalimu Nyerere, viongozi wa Mkoa wa Mbeya wataendelea kufanya kazi kwa bidii na kuwa wazalendo katika kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuwaletea maendeleo wananchi wa Mkoa huo.



Mkuu wa Mkoa wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera akizungumza na wanahabari wa Mkoa huo jana, kuhusu umuhimu wa kuuenzi Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioasisiwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere na kuizaa Tanzania **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbarali wahimizwa ulipaji wa bili za maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAKAZI wa Mtaa wa Isisi na Uhamila wilayani Mbarali , wamehamasishwa kulipa bili za maji ili kuiwezesha Mamlaka ya Maji ya Rujewa kutekeleza wajibu wake wa kuwahudumia wananchi.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Rujewa, Mhandisi Lestus Linda, wakati wa kukagua ukarabati wa tanki la maji la Isisi.

Alisema wananchi wanapaswa kulipa bili za maji kwa wakati badala ya kusubiri wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji kuwakatia huduma hiyo, huku akiwaahidi kuwasiliana na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutatua tatizo la umeme ili huduma ipatikane muda wote.

Mhandisi Linda aliongeza kuwa ukarabati wa tanki la maji Isisi lenye uwezo wa kuhifadhi lita za maji 90,000 ulifanyika baada ya tanki kuwa linavujisha maji hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa maji wakati wa kupampu pamoja na ongezeko la matumizi makubwa ya umeme ambao ulikuwa unasababisha kusukuma maji kwa muda mrefu ili kulijaza.

Aidha, alisema hadi sasa jumla ya wateja 119 wanapata huduma ya maji kupitia tenki hilo, na kwamba kiasi cha Sh. milioni saba kilitumika kukarabati tenki hilo.

"Kazi zilizotumika katika ukarabati wa tanki hili ni pamoja na kutindua ndani na nje ya tanki, kupiga plasta awamu mbili, kupiga niru ndani ya tanki pamoja na kupaka rangi na kuufanya mradi huo kufikia asilimia 98, kwa sababu tulianza kuutekeleza Januari 19 mwaka huu," alisema Mhandisi Linda.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alimpongeza Mhandisi Linda kwa kusimamia vyema ukarabati wa tanki la maji la Isisi na kwamba kumesaidia kuokoa upotevu wa maji.

Alisema kwa sasa wananchi wanaendelea kupata huduma za maji kwa uhakika kukilinganisha na ilivyokuwa awali ambapo maji yalikuwa ya mgawo.

# Nauli mpya ya bajaji ilivyoibua vilio Mbeya

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

BAADHI ya Abiria wanaotumia usafiri wa bajaji jijini Mbeya, wamesema wameshtushwa na uamuzi wa madereva wa vyombo hivyo kupandisha nauli kutoka Sh. 500 hadi 700.

Uamuzi wa kupandisha nauli ulitangazwa mwishoni mwa wiki iliyopita na uongozi wa bajaji jiji la Mbeya na kuanza kutekelezwa Jumatatu ya wiki hii.

Mmoja wa abiria, Tumaini Mwaipopo, mkazi wa Sabasaba, alieleza kushangazwa na uamuzi huo kwa kuwa walikuwa hawana taarifa zozote kwamba gharama ya nauli itapanda.

"Nimeshangaa nampa dereva bajaji Shilingi 1,000 cha ajabu ananirudishia chenji ya Sh.300 nilipomhoji ndo akaniambia kuwa nauli imepanda wakati mimi nilikuwa nategemea hiyo hela iniwezeshe kurudi nilipotoka, nimelazimika kutembea kwa mguu kutoka Mwanjelwa hadi Mzumbe,"alisema Mwaipopo.

Mwaipopo alishauri ni vyema wangepandisha nauli kwa kiwango cha sh. 600 kuliko kuweka 700 kwani gharama hizo zinaongeza makali ya maisha kwa wananchi hususani wakati huu ambao taifa linapitia kwenye mfumuko wa bei za bidhaa.

Sara Aliko, mkazi wa Sinde ambaye ni mchuuzi wa samaki alisema kupanda kwa gharama za nauli ya bajaji kutaathiri biashara yake kwa kuwa kila siku lazima akanunue kwa bei ya jumla kwenye Soko la Soweto na kila anapokwenda na kurudi anatumia usafiri wa bajaji.

Sara anahofia kuwa kutokana na mzunguko wake wa kila siku anaweza kutopata faida kwa sababu atalazimika kuchukua Sh. 400 kila siku kama fidia ya kiwango cha nauli kilichopanda kwa safari ya kwenda na kurudi.

Fodingo Allen, dereva wa bajaji alisema kuwa abiria wengi hawafahamu gharama mpya za nauli, hivyo wanaendelea kuwalekeza, lakini hawaachi kuwabeba wale wenye nauli ya zamani, akieleza kuwa bado hawajazoea.

"Sisi tulitaka iwe Shilingi 1,000, kutokana na gharama za vifaa na mafuta tunajikuta hela tunayoingiza kwa siku haikidhi mahitaji na malengo yetu ya siku," alisema.

Mwenyekiti wa wamiliki na madereva wa bajaji Jiji la Mbeya, Festo Mwasimba, alisema wameamua kupandisha nauli kutokana na kupanga bei ya vipuri na vifaa vya bajaji.

Alisema nauli ya zamani ya Sh. 500 imedumu kwa takribani miaka tisa, na kwamba kiwango hicho hakiendani na mahitaji pamoja na uendeshaji wa vyombo hivyo katika kipindi hiki.



## Wafanyakazi kujengewa mazingira bora kuleta ufanisi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Abdulla Suleiman, amesema serikali itahakikisha inajenga mazingira mazuri yatakayowawezesha wafanyakazi kufanya kazi katika kiwango bora ambacho kitaleta ufanisi wa kazi.

Abdulla alisema hayo wakati akifungua kongamano la Shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi (ZATUC), ambalo lengo lake ni kuwakutanisha wafanyakazi na kuzungumza changamoto zinazowakabili ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, Mei mosi.

Alisema, serikali katika kujenga mazingira mazuri kwa wafanyakazi wake, imeimarisha maslahi pamoja na haki zote wanazostahiki ikiwamo posho nje ya muda wa kazi.

Pia, alisema wamefanikiwa kujenga ushirikiano mzuri kati ya shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi na vyama vyao katika sehemu ya kazi hatua ambayo imeongeza uhusiano na kuleta ufanisi.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kuhakikisha mashirikiano mazuri yanakuwapo kati ya mwajiri na wafanyakazi katika sehemu za kazi hatua ambayo lengo lake ni kuleta ufanisi wa kazi na kuongeza uzalishaji wenye tija," alisema.

Hemed aliwataka wafanyakazi kuongeza ufanisi wa kazi na kuheshimu sheria za kazi ikiwamo kuepuka majungu na uzembe ambao ni chanzo kikubwa cha kuzorotesha utendaji wa kazi.

"Wakati serikali ikijipanga vizuri kuleta ufanisi wa kazi kwa kuimarisha maslahi bora tunawataka wafanyakazi kwa ujumla na wao wawe wabunifu ili kuyafikia malengo yanayotarajiwa," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa ZATUC, Khamis Mwinyi, ameitaka serikali kuwakemea baadhi ya watendaji waliokabidhiwa dhamana ya utendaji ambao hawapo tayari kutoa ushirikiano.

Alisema bado wapo watendaji wanaowakemea wafanyakazi wao na kuwabana kutoshiriki katika vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi kitendo ambacho kinakwenda kinyume na sheria za utumishi.

# Mwinyi: Miaka 58 Muungano unaendelea kuimarika zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa Muungano wa Tanzania ukiwa unatimiza miaka 58 bado unaendelea kuimarika.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo wakati akitoa salamu zake za miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kupitia vyombo vya habari, Ikulu Zanzibar.

Katika salamu zake hizo Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado wananchi wake wako pamoja hatua ambayo imeleta mafanikio makubwa ndani ya miaka 58.

Alisema, Tanzania bila ya Muungano sio kitu ambacho kinaweza kufikiriwa na Watanzania walio wengi wamezaliwa ndani ya kipindi cha Muungano na alitoa wito kwa wananchi wote kuendelea kuuenzi na kuudumisha kwa faida ya kizazi kilichopo na kijacho.

Aliongeza kuwa Muungano uliopo hivi sasa ni wa damu zaidi kuliko wa vitu kwa kuwa wananchi wengi wana uhusiano wa Zanzibar na Tanzania Bara na wote ni wamoja.

Rais Mwinyi alisema kwamba licha ya wananchi wake kuchanganya damu, pia kuna mafanikio makubwa yaliyopatikana kupitia Muungano hususan biashara na bidhaa nyingi zinazotumika Zanzibar zinatoka Tanzania Bara.

Alisema kuwa mbali ya muunganiko wa watu na biashara pia, kumekuwa na mafanikio makubwa katika suala zima la ulinzi na usalama na katika kipindi chote cha miaka 58 ya Muungano kumekuwa na amani na usalama.

Kadhalika, alisema mafanikio hayo yamepatikana kutokana na wananchi wenyewe kuwa ni watu wa amani pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na vikosi vya ulinzi na usalama ambavyo vinahudumia sehemu zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kwamba suala la Muungano lina nafasi kubwa katika Sera ya Uchumi wa Buluu ambayo ndiyo dira ya uchumi wa Zanzibar hasa ikizingatiwa kwamba eneo lote la bahari ni la Muungano ambayo pia, ni kiunganisho kati ya Zanzibar na Bara.

"Zanzibar kama kisiwa haiwezi kuleta maendeleo ikiwa peke yake tunawahitaji wenzetu na kwa kiwango kikubwa tunawahitaji wenzetu wa Bara kwa mambo yote yanayohusu uchumi wa buluu kwa mfano matumizi ya rasilimali za bahari kwenye uvuvi bahari yetu ni moja kwani eneo la uvuvi wa bahari ni la Muungano hivyo, bila shaka uchumi wa buluu utafanikiwa Muungano ukiendelea kuwapo," alisema Rais Mwinyi.

Alisema kuwa kunahitajika ushirikiano wa pamoja hasa katika matumizi ya rasilimali za bahari katika uvuvi kwa kuwa inaonesha wazi kwamba eneo lote la uvuvi wa bahari ni la Muungano na uchumi wa buluu utafanikiwa iwapo Muungano utaendelea kuwapo.

Alieleza kwamba bandari kubwa inayotarajiwa kuanzishwa Zanzibar kwa kiasi kikubwa itategemea biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na ni muhimu kuendeleza Muungano uliopo kwa manufaa ya pande mbili hizo.

Kadhalika, alisema ni muhimu kuendeleza Muungano kwa manufaa ya pande mbili za Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania na kusisitiza Zanzibar itafanya vizuri zaidi kiuchumi iwapo itaendelea kuwa katika Muungano.




Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Senyamule (kushoto), akipokea moja ya madawati 200 kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus kwa ajili ya shule za msingi Mchongomani, Bahari, Msufini na Mtakuja, mkoani humo juzi. NMB pia imetoa vitanda 10 na magodoro ya na mashuka 30 kwa ajili ya kituo cha Afya Katoro na viti 50 na meza zake kwa ajili ya Shule ya Sekondari Magenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatambua mchango wa KIST kuboresha vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, amesema serikali inatambua mchango wa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia (KIST), katika kuboresha maisha ya vijana na kulisaidia Taifa katika kuleta wataalamu wenye uwezo wa kukatua changamoto za kiufundi nchini.

Alisema Taasisi ya Karume inategemewa kwa kiasi kikubwa kufanikisha malengo ya sera ya nchi hususan katika maendeleo ya viwanda, sera ya uchumi wa buluu pamoja na ukuaji wa teknolojia.

Alieleza hayo wakati wa ufunguzi wa karakana ya matengenezo ya ndege inayojengwa katika taasisi hiyo, Mbweni Mjini Zanzibar, inayotarajiwa kutumiwa na wanafunzi wanaosoma fani ya uhandisi wa matengenezo ya ndege katika taasisi hiyo.

Alisema kuwa, hivi sasa dunia inategemea teknolojia katika harakati mbalimbali za maendeleo, na kwamba serikali inaendelea kuwa karibu na taasisi ya Karume ili kuhakikisha Zanzibar inaenda sambamba na dunia katika ukuaji wa teknolojia kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi kwa vitendo.

Alisema Serikali ya Zanzibar inakusudia kuboresha maisha ya Wazanzibari wote kwa vitendo na hilo linathibitishwa na sera zilizo bora na zinazotekelezeka za serikali.

"Tunategemea kwa kiasi kikubwa wahitimu wote watakaomaliza masomo yao katika taasisi hii katika fani ya uhandisi wa matengenezo ya ndege wataisadia serikali na watakuwa na uwezo wa kuajirika na mashirika mbalimbali nchini, na hata nje ya nchi," alisema.

Aliwaasa wanafunzi wanaotarajiwa kutumia karakana hiyo kutunza vifaa vilivyomo ili viweze kudumu kwa muda mrefu na vizazi vijavyo vinufaike.

Waziri Lela aliahidi kufanya jitihada za kina za kuhakikisha kuwa miradi mbalimbali itakayopatikana inaelekezwa katika taasisi za elimu ikiwamo Karume.

Naye Mkurugenzi wa KIST, Dk. Mahmoud Abdulwahab, alisema lengo la ujenzi wa karakana hiyo ni kuwawezesha wanafunzi wanaosoma fani ya uhandisi wa matengenezo ya ndege kujifunza kwa vitendo, kuhifadhi vifaa, pamoja na kutoa nafasi ya kutosha kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi hao.

Alisema, uwapo wa karakana hiyo katika taasisi utawawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira halisi yanayofanana na yale ambayo watakumbana nayo katika ajira zao baada ya kuajiriwa na ujenzi huo umezingatia masharti na vigezo.

Alifafanua kuwa mradi huo umbao umegharimu Sh. 362,143,791, umefadhiliwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), kwa kushirikiana na KIST ambayo ilitoa Sh. 62,143,791.

Aliishukuru TEA kwa kuufadhili mradi huo licha ya kuwapo changamoto wakati wa ujenzi, ikiwamo uadimikaji wa malighafi za ujenzi kama nondo, pamoja kuongezeka kwa bei ya badhi ya malighafi jambo lililosababisha kuongezeka kwa gharama za ujenzi huo.

Pia, alisema licha ya kuwapo kwa karakana hiyo, taasisi hiyo ina mpango wa kujenga jengo la ghorofa moja ambalo linaambatana na eneo karakana kwa ajili ya madarasa na ofisi ambazo zitatumika kuendesha mafunzo zaidi yanayohusiana na masuala ya usafiri wa anga.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Bahati Geuziye, alisema lengo la kufadhili mradi wa ujenzi wa karakana ya matengenezo ya ndege kwa ajili ya wanafunzi wa taasisi ya Karume ni kuongeza jitihada za serikali katika kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia ili kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake nchini.

Alisema kuwa, ufadhili uliotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Taasisi ya Karume, utasaidia kwa kiasi kikubwa jitihada za kuimarisha masomo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege kwa wanafunzi wa Tanzania.

"Usafiri wa anga ni muhimu katika kufanikisha jitihada za serikali za kupiga hatua zaidi kiuchumi kwasababu Tanzania kwa sasa inajielekeza kuwa nchi ya viwanda na uchumi wa kati," alisema.

Alifafanua kuwa, ili nchi iweze kupiga hatua kiuchumi ni lazima iwe na mfumo mzuri na ulio bora wa usafirishaji ikiwamo usafiri wa anga.

Pia, alisema kupitia ufadhili huo wa serikali vijana wengi watanufaika na kupata fursa ya masomo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege kwa gharama nafuu.

Alisema, Mamlaka inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio hayo, na kuahidi kuendeleza ushirikiano na taasisi za elimu katika uboreshaji wa mazingira ya kujifunza ili kufanikisha lengo la serikali la kutoa elimu bora kwa wananchi wake.

# Majaliwa: Wapokeeni wataalamu wa sensa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu yamefikia asilimia 81.

Aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa sherehe za miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, zilizohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kisiasa, kidini kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

Sherehe hizo zilibeba kauli mbiu isemayo 'Miaka 58 ya Muungano, uwajibikaji na uongozi bora, tushiriki sensa ya watu na makazi, anwani za makazi kwa maendeleo yetu'.

Majaliwa ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Maandalizi ya sherehe hizo, alisema: "Hadi kufikia jana (juzi) jioni, maandalizi ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi imefikia asilimia 81, Hivyo niwaombe Watanzania wajiandae kuwapokea wataalamu watakaopita kwenye makazi yao kutekeleza zoezi hilo."

Alisema kwa Mtanzania atakayeshindwa kuhesabiwa atakuwa amejinyima fungu lake katika mipango ya maendeleo nchini, kwa sababu sensa ni kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Kuhusu sherehe za maadhimisho ya miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza tukio hilo mwaka huu liendane na midahalo kwa vijana itakayokuwa na somo la kuelewa vizuri Muungano huo.

Alisema lengo la Rais Samia ni kuona midahalo ya Muungano itakayofanyika ihusu muungano na kila mmoja aweze kuona na kutambua kuwa urithi na tunu ambayo wameachiwa na waasisi wa Taifa inaendelezwa.

Katika sherehe hizo kulizinduliwa kitabu kiitwacho 'Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, chimbuko, misingi na maudhui' na kugawiwa kwa baadhi ya viongozi waliohudhuria sherehe hizo.

Vilevile, shehere hizo zilienda sambamba na utoaji wa mada mbalimbali kutoka kwa viongozi, akiwamo Spika wa Bunge Mstaafu, Pius Msekwa aliyetoa mada isemayo 'Historia, chimbuko, misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar'.

Akitoa mada hiyo, Msekwa alisema Aprili 22, 1964 kulifanyika mkataba wa makubaliano ya kuunda Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo yalisainiwa kati ya Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Abeid Amani Karume.

Msekwa alisema kulikuwa na usiri mkubwa kati ya viongozi hao wawili kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo kwa sababu ya kuhofia endapo mazungumzo yao yangejulikana mapema na maadui wangehujumu ili malengo yasitimie.

Msekwa alisema: "Hivyo viongozi hao wawili walikubaliana kufanya siri ya makubaliano hayo asifahamu mtu yoyote. Hata kazi ya kusaini kuligubikwa na usiri mkubwa."

Aliongeza kuwa: " Mwalimu Nyerere alipokwenda Zanzibar kuingia mkataba wa makubaliano hakuna mtu yeyote aliyefahamu, hata gazeti la serikali la kipindi hicho liliandika habari tofauti iliyoeleza kwamba Mwalimu Nyerere amekwenda Zanzibar kwa ziara ya kirafiki."

Msekwa alisema ukweli wa taarifa wa makubaliano ya mkataba huo yalianza kujulikana jioni baada ya wawili hao kuweka saini. Akisimulia zaidi, Msekwa alisema sehemu ya maudhui ya mkataba huo ilieleza kwanza Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa Mwalimu Julius Nyerere na Makamu wake atakuwa Abeid Aman Karume.

Alisema pia kulikuwa na orodha ya mambo 11 ya muungano, baadaye yaliongezwa hadi 22.

Alisema pia ilitengenezwa Katiba ya mpito ya Muungano na kukubaliana kwamba Katiba ya Tanganyika itakuwa ya mpito hadi pale itakapotengenezwa ya Jamhuri ya Muungano.




Ofisa Mtendaji wa Kampuni ya Smart Africa Group (SAG), Emmanuel Kaweda (kulia), akikabidhi msaada wa vyakula kwa Imam wa Msikiti wa Mtambani, jijini Dar es Salaam, Suleiman Abdallah (wa pili kushoto), vilivyotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya watoto yatima wanaolelewa na msikiti huo. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa SAG, Edwin Bruno. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Wanaogopa kuandika wosia wakiamini uchuro'

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI kuhusu wosia umebaini theluthi mbili ya watu hawana uelewa wowote kuhusu dhana hiyo na umuhimu wa uwekaji wosia huku baadhi yao wakiamini ni uchuro na suala linalohusu matajiri.

Utafiti huo ulioendeshwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), umegundua robo ya watu hawaoni haja ya kuandika wosia, kwa sababu wanaona hawana mali, huku wenzao wastani wa theluthi moja wakiona ni kitendo cha uchuro.

Hayo yamebainishwa kwenye Ripoti ya Haki za Binadamu 2021, iliyozinduliwa hivi karibuni jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, iliyojikita katika maeneo kadhaa ikiwamo haki za binadamu, kiraia na kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni na haki jumuishi.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kuhusu wosia na kugawanywa katika makundi sita, ilibaini asilimia 72 walisema hawako tayari sababu bado vijana, asilimia 63 walisema hapana wakidai ni uchuro na asilimia 76 wakidai hawawezi kuandaa sababu hawana mali za kutosha.

Aidha, asilimia 15 walisema wapo tayari kuandaa wosia kwa mdomo na si maandishi, huku asilimia 44 wakisema hawana uelewa kuhusu suala hilo.

Ripoti hiyo, imebainisha, wahojiwa kuhusu suala hilo katika mikoa mingi iliyofanyiwa utafiti mwaka 2021, baadhi ya wanajamii waliohojiwa walisema ikiwamo Geita, Mtwara na Kagera, walisema kuandika wosia sio kwa ajili yao, bali matajiri ambao wana mali nyingi.

"Watu hawataki kuandika wosia wakiamini ni kujichuria kifo. Wengine wanaamini wosia ni kwa ajili ya walio na mali nyingi," alijibu mmoja wa walioulizwa kuhusu suala hilo, mkoani Geita.

"Suala la kuandika wosia ni la watu wa mjini, kwa sababu wao ndio wasomi. Katika jamii yetu hapa kuandika wosia kunamaanisha kuanzisha migogoro ya kifamilia," alijibu mkazi wa mkoani Mtwara aliyeshiriki utafiti huo.

"Kuna wazee ambao wanaishi kwa hofu ya watoto wao wenyewe, wakijua kwamba wana uwezekano mkubwa wa kupigwa na watoto wanapogundua kuwa kuna wosia."

# ACT yapendekeza mambo 2 kwa Muungano

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimependekeza mambo makuu mawili kuhusu Muungano, ikiwamo mchakato wa haraka wa upatikanaji katiba mpya yenye mfumo imara wa Muungano pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha na kurejesha mamlaka stahiki kwa Zanzibar.

Msemaji wa Sekta ya Utumishi wa Umma, utawala bora na Muungano, Pavu Abdalla, alitoa mapendekezo hayo katika taarifa yake kuhusu miaka 58 ya Mungano wa Tanganyika na Zanzibar, inayoadhimishwa, leo.

Alisema wakati muungano wa Zanzibar na Tanganyika, ukitimiza miaka 58, ili kuondokana na mkwamo kuwa na haki na wa kuheshimiana na wenye furaha, chama hicho kimependekeza masuala hayo.

"Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ihakikishe kwamba mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha yanatekelezwa ikiwemo kuanzishwa kwake na kufanya kazi ipasavyo na kwa haraka Akaunti ya Pamoja ya Fedha.

"Irejeshe malimbikizo yote ya haki za mapato ya Zanzibar kutokana na mapato ya ziada ya Muungano kama ilivyochambuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha na kurejesha mamlaka kwa Zanzibar katika nyenzo muhimu za uchumi ikiwamo kodi, fedha, na ushirikiano wa kimataifa, ili Zanzibar iweze kujenga uchumi.

"Serikali ya Muungano kuipatia Zanzibar mgawo wake wa kifedha wa asilimia 11.02 kama ilivyowekeza katika mtaji wa uanzishwaji wa Benki Kuu ya Tanzania," alisema Abdalla kwenye taarifa hiyo.

Aliongeza kwamba ipo haja kuelekea miaka 59 ya Muungano kuzipa fursa pande mbili za Muungano ili ziweze kutumia vyema faida za sayansi na teknolojia na kuwapo mikakati bora ya kudumisha amani ya kweli na bila uhalifu.

"Ni miaka ya kuwa na mfumo bora wa Muungano kusimamia utekelezwaji wa haki za binadamu zikiwamo haki za misingi za kuchagua na kuchaguliwa na haki ya raia ya kutoa na kupokea habari, ili sauti ya kila mwananchi wa kila upande iweze kusikika".

HABARI KITAIFA

# DC awa mbogo kesi udhalilishaji Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja amesema, hatoivumilia familia yeyote itakayohusika na kusuluhisha kesi za udhalilishaji zinazotokea kwenye jamii.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi mkuu huyo alisema zipo baadhi ya familia hukimbilia kusuluhisha kesi mara tu baada ya mtoto wao kufanyiwa udhalilishaji, jambo ambalo siyo sahihi, kwani linachangia kuongezeka kwa vitendo hivyo.

Alisema kuwa, watakapoibaini familia yeyote ambayo mtoto wao amebakwa na kisha kusuluhisha bila kutoa taarifa mamlaka zinazo husika watawapeleka kwenye vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

"Kwa kweli familia zinazosuluhisha kesi za udhalilishaji zinarudisha nyuma juhudi zinazofanywa na serikali pamoja na taasisi binafsi katika kupiga vita vitendo hivyo, lakini sasa tutapambana vikali kuhakikisha tunadhibiti", alisema Mkuu huyo.

Alieleza kuwa, kati ya vipaumbele vya Wilaya ya Mkoani ni kuhakikisha wanapiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji sambamba na kuwachukulia hatua za kisheria wanaohusika kufanya matendo hayo.

"Hatuna muhali kwa hili, tunapopata taarifa ya mtoto ama mtu kufanyiwa udhalilishaji, tunasimamia kuhakikisha sheria inachukua nafasi yake", alieleza.

Mjaja aliwataka waananchi kuondosha muhali kwani ndio unaosababisha kuongezeka udhalilishaji na kupelekea kuvunja ustawi, heshima na utu wa mtoto ama mtu aliyefanyiwa kitendo hicho.

# Kikosi Kazi Katiba Mpya chaanza kupokea maoni leo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KIKOSI Kazi cha Rais, Samia Suluhu Hassan, kinachofanyia kazi masuala yanayohusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini kimeanza leo kupokea maoni na mapendekezo katika maeneo tisa ikiwamo Katiba Mpya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Kikosi kazi hicho, Sisty Nyahoza, kikosi kinapokea maoni hayo ya wananchi na taasisi mbalimbali kwenye maeneo ya mikutano ya hadhara na ya ndani ya vyama vya siasa.

Alitaja maeneo mengine ni masuala yanayohusu uchaguzi, mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa, ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Pia, maeneo mengine ni elimu ya uraia, rushwa na maadili katika siasa na uchaguzi, ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa, uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma.

Vile vile, alisema leo katika ukumbi wa Adam Sapi wa Ofisi ndogo ya Bunge mkoani Dar es Salaam, kikosi kitaanza kuongea na wadau mbalimbali wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kupokea maoni na mapendekezo yao.

"Ratiba ya kila wiki itakuwa inatolewa kwa umma, ili kuwakumbusha wahusika kuhusu mwaliko wa kuja kuongea na wajumbe wa kikosi kazi," alisema.

Alibainisha kuwa leo kikosi kitapokea maoni na mapendekezo kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu(LHRC), Jukwaa la Katiba (JUKATA) na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

"Aprili 28, mwaka 2022, watoa maoni na mapendekezo ni Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Kanisa la Sabato Tanzania, Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO)," alisema.

Kadhalika alisema Aprili 29, mwaka huu watapokea kutoka Baraza Kuu la Jumuiya na Taasisi za Kiislamu Tanzania, Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) na Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT).



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, wakiwa katika ziara kwenye Kiwanda cha mabati cha ALAF Tanzania, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, kwa ajili ya kujionea utendaji kazi wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mama wa Mbunge: Irene aliniambia anasikia kufa

**Na Jenifer Gilla**

MBUNGE wa Jimbo la Nsimbo, Anna Lupembe, ambaye ni mama wa marehemu aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Irene Ndyamkama, amesema kuwa kabla ya kifo cha mwanawe alimwambia kuwa anasikia kufa.

Aliyasema hayo jana katika misa ya kumuaga Irene iliyofanyika katika Kanisa la KKKT Usharika wa Segerea.

"Aliniambia mama nasikia kufa, nikamwambia hapana kataa hiyo roho ya umauti, akasema mama nasikia kufa na kweli akafa," alisema Anna kwa uchungu.

Alisema mwanawe alijifungua kwa operesheni ambayo ilikwenda vizuri na madaktari walifanikiwa kumtoa mtoto ambaye mpaka sasa yupo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na mama alifariki siku iliyofuata.

Mbunge huyo liongeza kuwa anamshukuru Mungu kwa ajili ya uhai wa mtoto wake kwa kuwa amemfundisha kuwa jasiri na kumpenda kila mmoja, japokuwa amemchukua, lakini amemuachia mkwe wake (mume wa marehemu) na wajukuu zake.

"Irene amenifundisha kuwa jasiri na kumpenda kila mmoja. Alikuwa anapenda watu, alisema mama usimnyanyapae mtu kwa kuwa kila mmoja ameletwa na Mungu. Alikuwa akikuona unamnyanyapaa mtu anakwambia sipendezwi na wewe," alisema.

Akisoma historia ya marehemu, Pendo Mpogole, alisema Irene alizaliwa Oktoba 15,1987. Alimaliza elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Bunge mwaka 1999. Akapata elimu ya sekondari nchini Uganda na kumaliza mwaka 2007.

Alipata elimu ya chuo kikuu nchini Marekani katika masomo ya biashara na kurudi nchini na kufanya shughuli za ujasiriamali.

Alisema Irene hakupata cheo cha ubunge wa viti maalum kama mtu binafsi bali alikuwa mwanachama wa Chama cha Mapinduzi tangu mwaka 2014 mpaka alipoteuliwa.

Aliongeza kuwa Irene alikuwa mtu wa watu, alihakikisha kuwa kila anayekutana naye anamfanya ajione kuwa ni wa muhimu.

"Mheshimiwa Irene alipenda kuongea na watu, alisikiliza kila mmoja aliyemhitaji. Nilikuwa namwita mama wa mikakati kwa sababu alipenda kupangilia mambo yake na aliyapa nafasi na muda wa kutosha," alisema.

Alisema historia ya marehemu aliyeacha mume na watoto watatu inamfanya atafakari kuwa maisha yake ni kitabu kinachoendelea kusomwa na jamii.

"Sisi kama familia, ndugu zake, marafiki zake, jirani zake bado tunaendelea kuyasoma maisha yake na kujifunza kupitia yale aliyoyatenda. Kwa hakika tunamshukuru Mungu kwa kuwa Bwana ametoa na Bwana ametwaa, Jina la Bwana lihimidiwe," alisema.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, alisema kuwa kifo cha Irene kimetokana na uzazi jambo ambalo nchi za Afrika zinakabiliana ili kumkinga mwanamke.

"Tunaomba katika nchi zetu za Afrika vifo vitokanavyo na kinamama vipungue kwa kuwa vinaua," alisema Kate.

Huku mwakilishi kutoka kampuni ya A and I Investment iliyokuwa inamilikiwa na marehemu, Diva Lupembe, alisema kuwa wamesikitishwa na kifo cha mbunge Irene kwa kuwa alikuwa ni kiongozi bora kwao.

Alisema kuwa marehemu hakuwa bosi wao tu bali alikuwa ni dada, rafiki, mama na msaada mkubwa kwao kwa kuwa alikuwa pamoja nao katika shida na raha na aliwaongoza vyema kama familia.

Naye Katibu wa Baraza la Ushirika wa Segerea, Obeid Mwangwa, alisema kuwa kanisa limepokea taarifa za msiba wa mbunge huyo kwa kuwa alilelewa na hata kufunga ndoa katika usharika huo, lakini hawana la kufanya kwa kuwa ni mapenzi ya Mungu.

Akizungumza mara baada ya misa hiyo Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Iringa, Rita Kabati, alisema bunge limepoteza mtu muhimu kwa kuwa alikuwa na upendo na mcheshi kwa kila mtu.

Naye Mchungaji mstaafu wa kanisa hilo, Kristophile Kalata alisema kuwa marehemu Irene alifanya kazi yake kuitumikia jamii kadiri Mungu alivyomuongoza na sasa kazi yake ameimaliza ni jukumu la waliobaki kuyaishi aliyoyatenda.

Alisema kuna wakati ambapo marehemu ilibidi atoe pesa yake mfukoni kusaidia wahitaji kwa sababu alikuwa mwaminifu kwa Mungu na alitii neno lake, na kuwa wito aliokuwa nao ulitoka kwa Mungu.

# MASHABIKI 24 'BETIKA MTOKO WA KIBINGWA' WAISUBIRI DABI

**Na Mwandishi Wetu**

MASHABIKI 24 wa Simba na Yanga keshokutwa, Ijumaa watawasili Dar es Salaam tayari kushuhudia bure mechi ya watani hao itakayopigwa Jumamosi Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya kushinda kwenye promosheni ya Betika Mtoko wa Kibingwa iliyofanyika kwa zaidi ya mwezi mmoja kote nchini.

Washindi hao 24 ambao ni mashabiki wa klabu kongwe za Simba na Yanga watashuhudia mechi hiyo bure kwa udhamini wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika.

Tayari washindi hao wamepatikana kwenye droo ya Betika Mtoko wa Kibingwa na wale kutoka nje ya Dar es Salaam wanatarajiwa kuwasili Ijumaa.

> **"Tumefunga pazia la droo ya Mtoko wa Kibingwa kwa kupata washindi wote 24," alisema Nelson Mwanuzi, Meneja Masoko wa Kampuni ya Betika.**

Aliwataja washindi hao kuwa ni Mbaraka Selemani wa Mtwara, Justine Bulaya (Arusha), Sifa Kaminyoge (Mbeya), Lameck Ndimugangwe na Edward Zakayo (Kigoma), Peter Martin (Singida), Leopord Thobias na Masatu John kutoka Mwanza.

Wengine ni Dismas Chilololoma wa Dodoma, Aaron Kulinga (Mbeya), Emmanuel Kivambe (Shinyanga), Boniface Molel (Manyara), Shafii Mgomi (Mtwara) na Raphael Kibifu wa Tabora.

Mwanuzi pia aliwataja washindi wengine kuwa ni pamoja na Emmanuel Zadie na Amos Mdao wa Dodoma, Sharafi Sharkati (Mtwara), Michael Richard, Patrick Ngwala na Ibrahim Kondo (Morogoro), Dominick Mwakalinga (Mbeya), Lameck Mbusiro (Mara), Hamis Omary (Tabora) na Furaha Juma wa Sumbawanga.

"Washindi kutoka nje ya Dar es Salaam wengi wao watawasili kwa ndege Aprili 29, mwaka huu na kuungana na wenzao ambapo Ijumaa watalala hoteli ya nyota tano wakiwa Dar es Salaam na kwenda uwanjani kushuhudia mchezo wa Simba na Yanga Jumamosi katika hadhi ya VIP," alisema.




Mmoja kati ya washindi 24 wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa', Dominic Mwakalinga, akionyesha mfano wa tiketi yake ya ndege tayari kwa safari ya kuelekea Dar es Salaam kushuhudia mchezo wa watani wa jadi, Simba na Yanga Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, gharama zote zikilipiwa na Kampuni ya Betika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Kichuya akunwa na ubora wa Mayele*

**Na Shufaa Lyimo**

WINGA wa Klabu ya Namungo FC, Shiza Kichuya amevutiwa na ubora unaoonyeshwa na mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, ambaye mpaka sasa amecheka na nyavu mara 12 katika Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kichuya alisema anavutiwa na aina ya uchezaji wa Mayele pamoja na juhudi zake anazoonyesha uwanjani mwanzo mwisho wa mchezo.

"Mayele ni mshambuliaji mzuri ambaye hakuna asiyeona nini anachokifanya, binafsi natamani kuwa kama yeye," alisema Kichuya ambaye alifunga bao pekee la Namungo wakati ikichezea kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumamosi iliyopita.

Kichuya alisema, Mayele akiwa uwanjani anajua jinsi ya kuutumia mpira jambo ambalo limemfanya ubora wake kuonekana katika kila mchezo.

Mbali na hilo, Kichuya alisema ataendelea kupambana kwa nguvu zote kuhakikisha anaiweka mahali pazuri timu yake ya Namungo ambayo kwa sasa ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 29, moja mbele ya Azam FC iliyopo nafasi ya nne lakini ikiwa nyuma mechi mbili.

Namungo imeshuka dimbani mara 21, huku Azam FC ikicheza mechi 19, na kila moja inawania kumaliza katika nafasi tatu za juu ili kukata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Tanzania itaingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

# Serikali yatoa neno Baseball, Softball

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, amewataka viongozi wa Chama cha Mchezo wa Baseball na Softball kuweka mikakati madhubuti kuelekea katika mashindano ya Afrika kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Julai mwaka huu nchini Mexico.

Mashindano ya Softball ya Afrika yanatarajiwa kufanyika Dar es Salaam kwa siku nne kuanzia Mei 32 hadi 26, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya kufanya mazungumzo na viongozi wa michezo hiyo, Neema alisema viongozi wanatakiwa kukamilishi masuala yote mapema ili kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa mafanikio makubwa.

Alisema ni heshima kubwa sana kwa Tanzania kupata nafasi ya uandaaji wa mashindano hayo makubwa jambo ambalo viongozi wanatakiwa kuweka mikakati vizuri ya kuendesha mashindano hayo huku Tanzania nayo ikihakikisha inafuzu kwenda kucheza Kombe la Dunia.

"Zimebaki siku chache kuanza kwa mashindano hayo, viongozi wanatakiwa kuhakikisha kila kitu kinaenda vizuri kwa kusimamia vema kambi ili kuendesha michuano hiyo bila kukwama," alisema Msitha.

Naye Katibu Mkuu wa Chama hicho, Alpherio Nchimbi, alisema maandalizi yanakwenda vizuri ikiwa ni pamoja timu ya wachezaji 13 kuingia kambini kwa ajili ya michezo hiyo.

"Kila kitu kinaenda vizuri na kuhusu maendeleo ya timu yetu iko kambini tangu Machi 2, mwaka huu kwa ajili ya maandalizi ya mashindano hayo, tunatarajia kufanya vizuri na kuwa miongoni mwa timu zitakazokwenda kucheza Kombe la Dunia," alisema. Nchimbi.

Alitaja nchi 10 zilizothibitisha kuja nchini kuwania tiketi hiyo, Mei 22, mwaka huu kuwa ni Kenya, Zambia, Misri, Tunisia, Uganda, Burkina Faso, Zimbabwe, Afrika Kusini na mwenyeji Tanzania.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RUDIGER KIMEELEWEKA REAL

REAL Madrid inakaribia kufikia makubaliano ya uhamisho kwa ajili ya mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger, 29, huku Mjerumani huyo akiwa tayari kuhamia Bernabeu kwa mkataba wenye mshahara wa angalau pauni 200,000 kwa wiki. ***(Guardian)***

### RICE ATAKIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inafikiria kumnasa kiungo wa West Ham na England, Declan Rice, 23, ambaye amekuwa akisakwa kwa muda mrefu pia na mahasimu wao Manchester United na Chelsea. ***(Telegraph)***

### MBAPPE NA HATIMA PSG

MSHAMBULIAJI wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 23, amekuwa akihusishwa na kutaka kuhamia Real Madrid katika majira ya joto, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa hatatangaza rasmi kuhusu hatma yake hadi baada ya mchezo wa mwisho wa klabu hiyo msimu huu dhidi ya Metz, Mei 21. ***(Marca)***

### SCOTT ASAKWA NORWICH

KLABU ya Norwich City imeingia katika mbio za kumsaka kiungo wa Bristol City, Alex Scott, 18, huku Tottenham na Leeds tayari zikimfuatilia kinda huyo. ***(Football League World)***

### BARCA KUMUACHIA DE JONG

BARCELONA wanaweza kukubali kumuachia Frenkie de Jong, 24, kuondoka kwa ada ya pauni milioni 58, huku Manchester United ikionesha nia ya kumtaka kiungo huyo wa Uholanzi. ***(El Chiringuito)***

### POGBA BAIBAI UNITED

MCHEZAJI ambaye ni wazi anaondoka pale Old Trafford ni Paul Pogba, 29, na tayari kiungo huyo Mfaransa ameshajiondoa kwenye kundi la WhatsApp la timu hiyo baada ya kupata ofa kutoka Madrid na PSG. ***(Mirror)***

### MESSI KUBAKI PSG

KLABU ya PSG itambakiza mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, 34, kwa msimu mmoja zaidi, lakini iko tayari kuruhusu mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye miaka 30 kuondoka. ***(Sky Sports News)***

### ORIGI AKARIBIA MILAN

AC Milan inakaribia kufikia makubaliano na mshambuliaji wa Liverpool, Divock Origi, 27. ***(Calciomercato)***

### DI MARIA NA JUVE

JUVENTUS ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga wa Argentina, Angel di Maria, 34, kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu baada ya kuamua kutoongeza mkataba wake. ***(Goal)***

### RASHFORD, DE JONG KUPISHANA

MANCHESTER United inaweza kuwapa Barcelona mshambuliaji wake wa kimataifa wa England, Marcus Rashford na mlinzi wa kushoto Mbrazil, Alex Telles, 29, ili kubadilishana na Frenkie de Jong. ***(Fichajes)***

### TEN HAG KUTATHMINI UNITED

KOCHA mpya wa Manchester United, Erik ten Hag atafanya mkutano wa mtandao na mchezaji mmoja mmoja kutathmini nani atabaki au kuondoka kabla ya kuanza kuinoa timu hiyo Juni. ***(Mirror)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# KANE: LAZIMA TUSHINDE MECHI TANO ZA MWISHO

**Tuna uwezo zaidi wa kufanya hivyo, tukishinda tano tutakuwa kwenye Ligi ya Mabingwa...**

**LONDON,** England

HARRY Kane amesisitiza kuwa Tottenham Hotspur lazima ishinde mechi zake tano zilizosalia za Ligi Kuu England, ili kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Spurs ya Kocha Antonio Conte inapigania nafasi ya nne na wapinzani wao wa jiji moja la London, Arsenal, ambao wako mbele kwa pointi mbili baada ya kuwalaza Manchester United 3-1 kabla ya Tottenham kubanwa na Brentford baadaye Jumamosi.

Hilo lilimaliza kipindi kibaya cha michezo miwili kwa kikosi cha Conte, baada ya kushindwa na Brighton and Hove Albion wakiwa nyumbani wiki iliyopita.

**Spurs pia walishindwa kupiga shuti hata moja lililolenga lango katika mechi zote dhidi ya Brighton na Brentford.**

Miamba hiyo ya London Kaskazini itakutana katika mechi iliyopangwa upya wiki ya mwisho ya msimu huu, ambayo inaweza kuamua nani atashika nafasi ya nne, na Kane amewataka Tottenham kukusanya pointi nyingi zaidi kutokana na michezo yao mitano iliyobaki.

Spurs watamenyana na Leicester City na Liverpool kabla ya kuhitimisha kampeni yao dhidi ya Burnley na Norwich City baada ya kukutana na 'Washikabunduki' hao wanaonolewa na Mikel Arteta, Mei 12.

"Kupata pointi moja pekee kutoka kwa mechi hizo mbili (Brighton na Brentford) inasikitisha," alisema Kane akiiambia Standard Sport.

"Tunakosa michezo katika suala la kushuka kwa pointi.

"Bado mechi tano zimebaki na tunahisi kwamba tutalazimika kushinda zote ili kupata nafasi hiyo. Tuna uwezo zaidi wa kufanya hivyo, tunaamini katika hilo na hilo ndilo tutajaribu kufanya.

"Je, bado iko mikononi mwetu? Ndio. Tukishinda mechi tano tutakuwa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuiangalia."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,198

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
VILLARREAL
1 | 1.26
X | 5.53
2 | 9.28

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BARCA HAIMUUZI DE JONG

**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa Barcelona, Jordi Cruyff amesisitiza kwamba, hawatamuuza Frenkie de Jong, ambaye amevutiwa na Manchester United.

Huku Kocha wa Ajax, Erik ten Hag, akitarajiwa kuhamia kule Old Trafford msimu wa majira ya joto, ripoti zimesema kwamba Mholanzi huyo anaweza kutafuta kuungana tena na De Jong pale United.

Kocha Xavi tayari amefanya kila awezalo kufuta uvumi huo, na sasa Cruyff amezungumza katika kujaribu kumaliza kabisa tetesi hizo.

"Hatutamuuza Frenkie de Jong, ni mchezaji anayethaminiwa sana ndani ya klabu," alisema Cruyff baada ya kufungwa na Rayo Vallecano, Jumapili.

Ahadi hiyo ya kumuunga mkono ilikuja kutokana na De Jong kuonekana kukosa utulivu baada ya Xavi kumtolea kauli.

De Jong mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akihusishwa na United na Bayern Munich katika miezi ya hivi karibuni.

Baba yake De Jong amemuunga mkono kuendelea na klabu ya Barcelona na hivi majuzi alikiri kiungo huyo hangependa hata kuhamia England kwa sababu ya hali mbaya ya hewa.



# Jesus: Mimi ni shabiki mkubwa wa Vinicius

**MACHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus amesema yeye ni "shabiki mkubwa" wa Vinicius Junior anayekipiga kule Real Madrid.

Timu hizo jana, Jumanne usiku zilikutana kwenye nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Jesus, ambaye alikuwa Mbrazil wa kwanza kufunga mabao manne katika mechi moja ya Ligi Kuu England wakati City ilipoibomoa 5-1 Watford, Jumamosi, analenga kuwasaidia vijana hao wa kocha Pep Guardiola kutwaa taji la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kupoteza fainali ya msimu uliopita dhidi ya Chelsea.

Mchezaji mwenza na Jesus kwenye timu ya Taifa ya Brazil, Vinicius amehusika katika mabao 31 akiwa na Real Madrid katika mashindano yote msimu huu (mabao 17, asisti 14), na vijana hao wa Kocha Carlo Ancelotti wanawania taji la 14 la Ulaya.

Akikumbuka mchezo wa mwisho wa Man City wa Ligi ya Mabingwa
Ulaya dhidi ya Madrid
tika hatua ya 16-bora
2019-20, ambao alifu
mabao katika miguu y
miwili ya ushindi wa ju
la wa 4-2, Jesus amese
kuibuka kwa wache
kama Vinicius kunaup
ba mchezo huo.

"Ilikuwa ngumu s
na ya wasiwasi, ka
kawaida unapoch
Bernabeu dhidi ya R
Madrid," alisema Je
akiliambia gazet la Ma

"Mimi ni shabiki mk
wa wa Vinicius, natuma
ataendelea kuwa bora
bora siku zijazo. Namta
mafanikio mema.

3,475,840

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/04/22 | 17:00 | Watford vs Burnley | 2.51 | 3.20 | 2.71 |
| 02. 30/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Brighton | 2.64 | 3.04 | 2.69 |
| 03. 30/04/22 | 17:00 | Southampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.26 | 2.97 |
| 04. 30/04/22 | 17:00 | Barnsley vs Preston | 2.77 | 3.27 | 2.42 |
| 05. 30/04/22 | 17:00 | Coventry vs Huddersfield | 2.52 | 3.17 | 2.72 |
| 06. 30/04/22 | 19:00 | Sampdoria vs Genoa | 2.46 | 3.18 | 2.79 |
| 07. 30/04/22 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Atletico Madrid | 2.95 | 3.05 | 2.48 |
| 08. 01/05/22 | 15:00 | Elche vs Osasuna | 2.99 | 3.09 | 2.42 |
| 09. 01/05/22 | 15:30 | GO Ahead Eagles vs Vitesse Arnhem | 2.59 | 3.43 | 2.49 |
| 10. 01/05/22 | 16:00 | Empoli vs Torino | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 11. 01/05/22 | 17:15 | Granada vs Celta Vigo | 2.56 | 3.16 | 2.76 |
| 12. 01/05/22 | 19:30 | Rayo Vallecano vs Real Sociedad | 2.96 | 3.06 | 2.47 |
| 13. 01/05/22 | 21:00 | Waalwick vs Groningen | 2.68 | 3.33 | 2.46 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA

"X" - NI TIMU KUTOKA SARE

"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 27/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1881 | Oita Trinita vs Tochigi SC | 1.96 | 3.02 | 3.89 |
| 13:00 | 4006 | Tokushima Vortis vs Montedio Yamagata | 2.43 | 3.01 | 2.81 |
| 13:00 | 4546 | Roasso Kumamoto vs Vegalta Sendai | 2.66 | 3.05 | 2.52 |
| 13:00 | 5279 | Yokohama vs Machida Zelvia | 2.24 | 3.02 | 3.11 |
| 13:00 | 5649 | Niigata Albirex vs Grulla Morioka | 1.69 | 3.30 | 4.86 |
| 13:30 | 2618 | Ventforet Kofu vs Tokyo Verdy | 2.31 | 3.12 | 2.88 |
| 15:30 | 1277 | AEK Athens B vs Kifisias | 2.93 | 3.22 | 2.23 |
| 15:30 | 2918 | Ergotelis vs Irodotos | 11.66 | 3.45 | 1.38 |
| 15:30 | 3212 | Almopos Arideas vs Panserraikos | 7.20 | 3.89 | 1.42 |
| 15:30 | 3356 | Kissamikos vs O F Ierapetras | 2.32 | 2.32 | 4.80 |
| 15:30 | 3509 | Niki Volou vs Olympiacos Piraeus B | 2.05 | 3.35 | 3.50 |
| 15:30 | 4646 | Pierikos Katerini vs Anagennisi Karditsas | 1.58 | 3.45 | 5.63 |
| 15:30 | 4664 | Olympiakos Volos vs Apollon Larisas | 7.22 | 4.58 | 1.35 |
| 15:30 | 5397 | Karaiskakis vs Levadiakos | 2.97 | 3.21 | 2.22 |
| 17:00 | 3290 | Sokol Ostroda vs Pogon Siedlce | 4.00 | 3.50 | 1.86 |
| 18:00 | 1027 | Lamia vs Panathinaikos | 4.86 | 3.60 | 1.62 |
| 18:00 | 2701 | Radunia Stezyca vs Slask Wroclaw II | 1.78 | 3.66 | 3.76 |
| 18:00 | 3288 | Vyskov vs Graffin Vlasim | 3.31 | 3.17 | 2.07 |
| 18:00 | 4165 | Orlando Pirates vs Chippa Utd | 1.65 | 3.32 | 5.74 |
| 18:00 | 4324 | PKS Olimpia Elblag vs Znicz Pruszkow | 2.01 | 3.25 | 3.75 |
| 18:00 | 4806 | SK Prostejov vs Taborsko | 2.11 | 3.24 | 3.15 |
| 18:00 | 4905 | FK Viktoria Zizkov vs Opava | 3.51 | 3.31 | 1.95 |
| 18:00 | 5264 | Pribram vs MFK Chrudim | 1.96 | 3.26 | 3.55 |
| 18:00 | 5473 | Usti Nad Labem vs Dukla Prague | 3.00 | 3.25 | 2.33 |
| 18:00 | 5575 | Sparta Prague B vs Jihlava | 1.67 | 3.60 | 4.47 |
| 18:15 | 3787 | Wigry Suwalki vs LKP Motor Lublin | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 19:00 | 1364 | Fiorentina vs Udinese | 1.67 | 3.82 | 4.57 |
| 19:00 | 2069 | Wisla Pulawy vs Ruch Chorzow | 3.50 | 3.25 | 2.10 |
| 19:00 | 3270 | SV Lippstadt 08 vs VfB Homberg | 1.45 | 4.20 | 5.86 |
| 19:00 | 5149 | KS Gornik Polkowice vs GKS Jastrzebie Zdroj | 2.07 | 3.17 | 3.32 |
| 19:00 | 5325 | GKS Katowice vs Skra Czestochowa | 2.03 | 3.30 | 3.30 |
| 19:15 | 2808 | Ansbach vs 1 FC Sand | 1.10 | 8.14 | 15.51 |
| 19:30 | 1786 | Rapid Vienna vs Austria Klagenfurt | 1.45 | 4.28 | 5.65 |
| 19:30 | 4378 | Sturm Graz vs RB Salzburg | 4.49 | 3.80 | 1.63 |
| 19:30 | 5415 | Wolfsberger AC vs Austria Vienna | 2.18 | 3.30 | 2.96 |
| 20:00 | 1619 | ZKS Stal Rzeszow vs KS Hutnik Krakow Ssa | 1.30 | 5.24 | 7.18 |
| 20:00 | 3177 | Sonderjyske vs Odense | 2.57 | 3.05 | 2.61 |
| 20:00 | 4218 | Bayern Munchen II vs Buchbach | 1.20 | 6.22 | 9.72 |
| 20:00 | 4945 | Zbrojovka Brno vs Fotbal Trinec | 1.25 | 5.27 | 9.17 |
| 20:00 | 5578 | Olympiakos vs PAOK | 1.88 | 3.20 | 4.40 |
| 20:30 | 1029 | Mamelodi Sundowns vs Cape Town City | 1.49 | 3.86 | 6.74 |
| 20:30 | 2524 | ROT Weiss Ahlen vs Alemannia Aachen | 2.67 | 3.31 | 2.36 |
| 20:30 | 4401 | Chojnice vs Lech II Pozna | 1.61 | 3.66 | 4.88 |
| 21:15 | 5030 | Bologna vs Inter | 6.74 | 4.86 | 1.38 |
| 21:15 | 5350 | Atalanta vs Torino | 1.59 | 3.98 | 4.98 |
| 21:30 | 5667 | Arka Gdynia vs LKS Lodz Pss | 2.02 | 3.30 | 3.30 |
| 21:45 | 1854 | Middlesbrough vs Cardiff | 1.57 | 3.82 | 5.55 |
| 22:00 | 4517 | Liverpool vs Villarreal | 1.26 | 5.53 | 9.28 |
| 22:30 | 3010 | Al Ahly Cairo vs Talaea El Gaish | 1.34 | 4.56 | 9.13 |
| 22:30 | 4787 | Pyramids vs Ceramica Cleopatra | 2.16 | 3.00 | 3.60 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# RAGE, KIBADENI WATAKA MASTRAIKA WAPYA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI, viongozi na makocha wa zamani wa klabu ya Simba, Ismail Aden Rage na Abdallah Kibadeni wameipongeza Simba kwa hatua iliyofikia ya robo fainali licha ya kutupwa nje na Orlando Pirates ya Afrika Kusini Jumapili iliyopita, wakitaka mabadiliko makubwa yafanyike kwenye kikosi, hasa upande wa ushambuliaji, huku Kocha Mkuu Pablo Franco akipigiwa upatu asalie kwenye kikosi hicho.

**Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wakongwe hao walionyesha kuumia kwa timu yao kutolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 kwenye Uwanja wa Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini, lakini wakiwapongeza wachezaji wa timu hiyo kwa kupambana hadi dakika ya mwisho.**

Simba ilitolewa kwa penalti, baada ya kufungwa bao 1-0, huku pia ikishinda idadi hiyo ya bao nyumbani, hivyo timu hizo kwenda sare ya bao 1-1 kwa dakika 180.

"Tatizo letu bado wamaliziaji pale mbele ni butu, kuna mabadiliko yanapaswa yafanyike kwenye eneo hilo, nasikia pia mkataba wa kocha, sina hakika ila nasikia ilikuwa ni kuifikisha nusu fainali, hakufika ila nashauri wangemuacha hata mwaka mmoja na nusu tuone uwezo wake.

"Kiufundi siyo kocha mbaya, mimi nimepata bahati ya kuwa mchezaji, kuongoza soka kuanzia klabu mpaka timu ya taifa na pia nimehudhuria mafunzo ya mpira wa miguu, nikisema kocha huyu anafaa ujue anafaa," alisema Rage ambaye aliwahi kuichezea timu ya Simba na kuiongoza kwa vipindi tofauti, pia kukiongoza Chama cha Soka nchini wakati huo FAT, kabla ya kuwa Shirikisho.

Naye mchezaji wa zamani wa timu hiyo aliyecheza kwa mafanikio na kuwa kocha wa mafanikio pia, Kibadeni, alisema ameumia kwa Simba kutolewa kwenye michuano hiyo ya kimataifa, kwani alitegemea kuwa ingevuka hatua hiyo.

"Tunasikitika hatukufikia malengo, tulitegemea tungevuka zaidi ya hapo, lakini huo ndiyo mpira kwa sasa ni kujipanga, Simba bado nafasi inayo ya kufanya vizuri tena kimataifa. Ukiangalia 'plan' (mpango) walioingia nao ni mzuri, lakini ulikwama, wachezaji walicheza vizuri kiasi, lakini walizuia sana kuliko kushambulia, nadhani wangeanza kutafuta goli moja kwanza," alisema Kibadeni.

Alishauri timu hiyo itafute mastarika ambao watairahisishia kazi kwenye michuano kama hii kama wanatafuta angalau bao moja la ugenini.

Kikosi cha Simba kiliwasili juzi usiku nchini kikitokea Afrika Kusini na sasa kinajiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Yanga, Jumamosi wiki hii kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.



# Yanga Princess yatamba kuendeleza moto




**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kufanikiwa kuifunga Simba Queens kwa mara ya kwanza katika historia yake tangu ianze kucheza Ligi Kuu ya Wanawake kwa msimu wa tatu sasa, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema lengo lao ni kuendelea na mchezo huo kwa kupata pointi tatu katika kila mechi iliyopo mbele yao.

Katika mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili iliyopita, Yanga Princess ilibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Simba Queens ambayo ilicheza pungufu kwa dakika 85 baada ya beki wao wa kati, Juliet Singano kutwangwa kadi nyekundu dakika ya tano, kutokana na kuinua mguu juu uliotua kichwani kwa mchezaji wa wapinzani wao, Lucia Mrema.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Edna alisema moto waliouwasha dhidi ya Simba Queens watauendeleza kwenye michezo mingine.

"Sasa hivi moto umewaka, tutaendelea kuuwasha kwenye michezo mingine iliyopo mbele yetu," alisema Edna ambaye pamoja na ushindi huo timu yake bado inazidiwa kwa alama saba na watani wao hao wa jadi.

Kocha huyo alisema katika mchezo wao huo uliopita, wachezaji walionyesha kiwango cha hali ya juu kitu ambacho kinampa matumaini ya kuendelea kufanya vizuri.

Alisema licha ya kupata pointi tatu katika mchezo huo ambao ulikuwa na ushindani mkubwa, kuna makosa madogo madogo ya kiufundi aliyoyabaini na ameahidi kuyafanyia kazi kabla ya kushuka tena dimbani.

Edna alisema amefurahi sana kuweka historia ya kuifunga Simba Queens kwa mara ya kwanza tangu timu yake ipande Ligi Kuu.

Michezo

Jumatano Aprili 27, 2022

Nipashe



Kane: Lazima tushinde mechi tano za mwisho UKURASA 21

# Simba: Ushindi Yanga si dawa maumivu CAF

## ●●● Pablo asema ni ngumu kusahau, lakini wanatakiwa kusonga...

**Na Saada Akida**

WAKATI watani wao wa jadi, Yanga wakielekeza nguvu kubwa katika mechi ya 'dabi' Jumamosi, Klabu ya Simba imesema licha ya ukweli kwamba sasa wanageukia mechi za Ligi Kuu zilizopo mbele yao ikiwamo hiyo, lakini hata kama watashinda dhidi ya watani zao hao, ushindi huo hautaweza kuwaondolea maumivu na uchungu wa kupoteza dhidi ya Orlando Pirates.

**Simba ambayo Jumamosi itakuwa ugenini kuivaa Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Jumapili iliyopita ilitolewa na Orlando Pirates kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-3, kwenye mechi ya robo fainali mkondo wa pili ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini, ilimalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0, kama ilivyokuwa mechi ya mkondo wa kwanza dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 1-1, ndipo mikwaju ya penalti ikachukua nafasi yake na Simba kutolewa.

Akizungumza na gazeti hili juzi baada ya Simba kutua nchini wakitokea Afrika Kusini, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo alisema wachezaji wake walipambana na haikuwa bahati kwao na sasa wanahamishia nguvu zao mchezo ujao dhidi ya Yanga na mingine.

Alisema malengo yao yalikuwa kufika nusu fainali, lakini habati haikuwa upande wao, hivyo kwa sasa wanasahau matokeo ya nyuma na kujiandaa na michezo iliyopo mbele yao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanaendea kutafuta pointi muhimu dhidi ya wapinzani wao.

"Ni ngumu kusahau, lakini tunatakiwa kusonga mbele, sasa ni muda wa kuweka akili zetu katika mchezo dhidi ya Yanga, tunahitaji kupambana kuhakikisha tunapata ushindi katika mchezo huo," alisema Pablo.

Meneja wa idara ya habari na mawasiliano wa Simba, Ahme Ally, alisema wamerejea nyumbani kwa ajili ya michuano ya FA na Ligi Kuu, na mechi iliyopo mbele yao ni Jumamosi dhidi ya Yanga.

Alisema wanahitaji kufanya vizuri katika mchezo wao huo kwa kuwafunga Yanga ili kulinda heshima ya Derby na kupata pointi tatu mbele ya wapinzani wao hao haitafuta machungu ya Simba kuondolewa Shirikisho.

"Kushinda mbele ya Yanga ni jambo kubwa, lakini halitaweza kufuta machungu ya kupoteza malengo yetu ya kucheza nusu fainali, kuna tofauti kubwa sana kulinganisha mchezo dhidi ya watani wetu na Kombe la Shirikisho.

"'Level' ya thamani ya kuipoteza fainali ya Kombe la Shirikisho na 'level' ya tamani ya kuifunga Yanga ni mbingu na ardhi, hata tukiifunga bao 100, machungu ya Wanasimba (kupoteza robo fainali) hayatafutika," alisema na aliongeza;

"Tutakapomfunga Yanga mashabiki wetu watafurahi kwa sababu tumepata pointi tatu na kumfunga mpinzani wetu, ila haitafuta machungu yetu tuliyojiwekea msimu huu kucheza nusu fainali."

Alisema wanashukuru wamerejea salama na hawajafurahishwa na matokeo licha ya kuwafariji kutokana na historia ya nyuma ya kuondolewa katika mashindano hayo.

Ahmed alisema msimu wa kwanza na pili walitolewa katika hatua ya robo fainali kwa kufungwa idadi ya mabao mengi ikiwamo manne, ila safari hii wanepiga hatua ya kuondolewa katika mikwaju ya penalti.

"Ukiangalia hapo kuna mabadiliko makubwa, Simba imepiga hatua kubwa kwa sababu tulitamani kutinga nusu ila tumeishia robo, malengo hayakutimia, lakini tumetimiza majukumu.

"Wachezaji wamefanya majukumu yao, kila mmoja amefanya kile alichopaswa kufanya kutolewa kwetu tunepata funzo na kujipanga kwa msimu ujao , kuendelea hapa tulipoishia na kupiga hatua mbele zaidi," alisema Meneja huyo.

Msemaji wa Yanga, Haji Manara amesema kikosi chao kipo fiti kwa ajili ya mchezo huo na jana kiliingia kambini kujiandaa zaidi.

"Baada ya mechi na Namungo tuliwapa mapumziko wachezaji wetu, na leo (jana), wataingia kambini kwa maandalizi zaidi," alisema.

MASHUJAA...



Wachezaji wa Simba wakirejea nchini wakitokea Afrika Kusini, ambapo walitolewa na Orlando Pirates kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-3 baada ya matokeo ya jumla nyumbani na ugenini kuwa 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Kichuya akunwa ubora wa Mayele

**Na Shufaa Lyimo**

WINGA wa Klabu ya Namungo FC, Shiza Kichuya amevutiwa na ubora unaoonyeshwa na mshambuliaji wa Yanga, Fiston



HABARI UK 20



## Barca yaigomea Utd kwa De Jong

**BARCELONA,** Hispania

MKURUGENZI wa Barcelona, Jordi Cruyff amesisitiza kwamba, hawatamuuza Frenkie de Jong...

HABARI UK 22

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >